

TARAJIO

 Habari za jioni, marafiki. Bila shaka ni majaliwa kurudi tena, usiku wa leo, huku Long Beach kuwa na wakati huu wa ushirika katika majuma yajayo. Na kwa namna fulani ilinishtua kujua kwamba ningekaa Long Beach kwa muda huu mrefu, ulioongezewa.

² Nami nafikiri Ndugu Arganbright, aliponipigia simu kuhusu kuja Pwani ya Magharibi kutoka Phoenix, aliomba usiku mmoja huko Los Angeles, na usiku mmoja hapa, na ndipo ninapoona ya kwamba ninao, ama, usiku mmoja, ninamaanisha juma moja kila mahali, samahani, halafu nikaona nina majuma mawili hapa, Jumapili hadi Jumapili, nafikiri ndivyo, ama, Jumanne hadi Jumapili, hadi Jumapili. Na kwa hiyo, tunatarajia sasa, kuwa na wakati mzuri sana. Sasa, tunaweza tu kuwa na wakati mzuri katika Bwana, tunapomwabudu Yeye pamoja, hatuna budi kufanya hivyo.

³ Na sasa, nilikuwa nikizungumza na mchungaji, leo, ndipo—ndipo nikamwuliza ni ibada ya aina gani, tulikuwa tukitarajia uamsho, au alikuwa afanye ibada ya uponyaji? Naye akasema, “Kama tu Bwana atakavyoongoza.” Kwa hiyo hilo, ni zuri tu nadhani, kadiri ningaliweza kuomba. Hilo ndilo tunalotaka, tunataka mahali Bwana anapoongoza, na halafu kama Bwana ana nafasi ya kwanza, basi kila kitu kitakuwa sawa.

⁴ Na ni, nafikiri hii ni mara yangu ya pili kwenye maskani hii. Nafikiri hapa ndipo mahali tulipokuja, sivyo Ndugu Demos, usiku mmoja hapa chini, yapata miaka miwili ama mitatu iliyopita, ama kitu fulani? Na, miaka kadhaa iliyopita, naam, bwana. Na halafu wakati mmoja nilikuwa huko kwenye Ukumbi wa Manispaa hapa wakati sisi, nilipokuja kwa mara ya kwanza Pwani ya Magharibi, na kwa hiyo kwa namna fulani kwanza kabisa ninajisikia kana kwamba mimi ni sehemu yenu, si kwa sababu tu nimekuwa hapa, kwa sababu nimekuwa mahali pale pale mlipopata wokovu, pale Kalvari. Na hapo ndipo sisi... Chemchemi pekee niujuayo ni ile Chemchemi ya Kalvari, ambapo Mungu alimwaga baraka Zake juu ya jamii ya binadamu, na hapo ndipo nilipopokea zangu, chini ya Damu ya Bwana Yesu.

⁵ Na sasa, Bwana akipenda, ningetaka tu kuona ni wangapi waliokuwa wanataka kuombewa, tufanye ibada ya uponyaji usiku mmoja. Hebu tuone kama tukiinua mikono yetu, huku. Vema, hilo ni kundi dogo zuri kwa ajili ya ibada ya uponyaji, kwa hiyo, kwa ajili ya kanisa, kwa vyovyote vile.

⁶ Halafu basi, vema, kesho usiku, mngetaka kuwa na ibada ya uponyaji namna gani kesho usiku, hilo lingekuwa sawa? Vema, nitawaagiza wavulana hapa wasambaze kadi za maombi yapata

saa kumi na mbili u nusu, kitu kama hicho, isiye ikaingilia sehemu zingine za mkutano. Ndipo basi tutawaombea wagonjwa kesho usiku, Mungu akipenda.

⁷ Na ndipo tutaona basi wakati akiongoza, tunapoendelea, tuone ni wangapi. . . Mnajua katika mkutano mdogo wa kanisa kama huu, tunaweza kuwaombea wagonjwa wote katika usiku mmoja. Kwa hiyo, kuwa hapa siku kumi na tatu usiku, hiyo itakuwa—itakuwa ni ibada kwelikweli ya uponyaji. Kwa hiyo, kama watu wakiingia, wagonjwa wanaendelea kusongamana ndani, mbona, tutaendelea kuwaombea wa—wanapoingia.

⁸ Sasa, labda juma hili lijalo, juma hili lingine lijalo, hasa, yakiwa ni mapenzi ya Bwana, ndio kwanza nimalize, kabla sijaanza ziara ya mwaka huu, kwenye maskani yangu, nilimaliza mfululizo wa nyakati saba za mwisho za kanisa katika Ufunuo. Na labda, Bwana akipenda, ningetaka kuchukua juma lijalo juu ya wale wapanda farasi wanne wa Ufunuo, na kutoa usiku mmoja kwa kila farasi na kila mpanda farasi, na kile anachowakilisha katika wakati tunaishi.

⁹ Nafikiri i—inapswa kuwa sote tunapaswa kuonywa juu ya mambo yajayo. Hilo ndilo kanisa siku hizi limepungukiwa, ni onyo la kujiweka tayari. Ninaamini, kwa kweli, kanisa lilikuwa katika hali bora miaka arobaini iliyopita kwa ajili ya kuja kwa Kristo kuliko lilivyo leo, miaka arobaini.

¹⁰ Nilikuwa nikizungumza juu ya jambo hilo hivi majuzi huko Westward Ho, kwenye Mkutano wa Wafanyabiashara wa Full Gospel, jinsi ambavyo kanisa, katika miaka arobaini, lilivyorudi nyuma, kama tu lilivyofanya huko nyikani, lakini ni wakati sasa ambapo wale wapiganaji wa kale wamekufa, nasi tunapaswa kukusanyika pamoja, na kuanza kusonga mbele kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, na kuvuka ng'ambo na kumiliki baraka zote.

¹¹ Na kama tu vile Bwana atakavyoongoza juma hili, tutakuwa tukizungumza juu ya masomo hayo, katika kujiweka tayari.

¹² Sasa, mhudumu hawezi kuleta uamsho, hakuna mhubiri anayeweza kuleta uamsho, yeye haubebi, na jambo pekee analoweza kufanya ni kuwa tu mwaminifu kwa Mungu na Neno Lake, nao uamsho hauna budi kupitia kwa watu, nyumbani mwako, maishani mwako. Sasa, *uamsho* si kuongeza washiriki wapya kanisani, ni kuwaamsha wale tulio nao tayari, *kuamsha* maana yake ni “kurudisha.” Kwa hiyo uamsho. . .

¹³ Nilisimama, hapa miaka kadhaa iliyopita, kwa mara yangu ya kwanza karibu na eneo kubwa la maji, ambalo lilikuwa ni Ziwa Michigan, nilikuwa karibu, ilikuwa ndio kwanza nitawazwe katika Kanisa la Kimishenari la Kibaptisti, nilikuwa na umri wa kama miaka ishirini ama ishirini na mmoja. Nami nilikuwa nimepanda kwenda kule walipokuwa na, walikuwa na ibada kuu ya mapambazuko ya Pasaka huko kando ya ziwa.

¹⁴ Nami nilimfahamu Paul Rader, naye alitarajiwa kuzungumza kwenye mkutano huo, nami nilitaka kutembelea hayo maskani nilipokuwa Chicago. Na ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kuona eneo hilo kubwa la maji.

¹⁵ Ndipo nikatoka nje kwenye Barabara ya Ufuo wa Ziwa na kusimama huko nje kidogo, nami nikaona mawimbi hayo yote yakirukaruka, yaki—yakirushwa—rushwa tu kote, nikawaza, “Mbona kulisimkwa hivi? Msisimko huu wote ni wa nini?”

¹⁶ Ndipo mawimbi madogo yangeanza, kisha yanaenda huko, na kuwa mawimbi makubwa mno, na kugongana, yanaachana, na—nalo povu lingeruka juu, kisha lingerudi ndani, ndipo naona mawimbi makubwa yakija tena, yakiishia ukingoni, kama mlivyozoea hapa, lakini hilo lilikuwa ni jambo jipya kwa—kwangu mimi, m—m—mtumishi wa bara. Kwa hiyo, niliona jinsi yungeninii. . .

¹⁷ Ndipo nikasema, “Vema, hapana shaka, ziwa lina uamsho, hapana shaka ndivyo ilivyo, lina wakati mzuri, kurukaruka tu juu chini.” Nikawaza, “Hilo ni—hilo ni zuri, hilo ni sawa.”

¹⁸ Lakini, mwajua, ni—niliwaza, “Vema, sijui kama linapata maji mengi ya ziada wakati linapokuwa na uamsho?” Nikawazia, “La, hakuna tone moja zaidi ndani yake, sasa hivi, kuliko kama lilikuwa shwari kabisa, hata moja. Ni maji yale yale, bali yakiwa tu na uamsho, yakirukaruka.” Nikawaza, “Vema, hilo linaleta faida gani?”

¹⁹ Kumbé, wakati linapokuwa na uamsho, na kuruka juu chini namna hiyo, linafagilia mbali takataka zote kutoka kwake hadi ufukoni. Kwa hiyo hicho ndicho Kanisa linachohitaji, ni uamsho, kufagilia mbali ulimwengu wote na mambo ya ulimwengu, lipate kuonekana safi, kuwa zuri tena. Wakati lote limetulia, lina kiasi kile kile cha maji.

²⁰ Lakini kinachoifanya bahari kufanya hivyo, ni kwa sababu kuna upepo unaokuja, unaanza kuvuma dhidi ya mawimbi, unavuma kwenye hilo eneo la maji mengi, unayainua. Vema, huo ndio Kanisa linahitaji usiku wa leo, ni Upepo wenye Nguvu Unaenda kasi ukishuka juu Yake tena, na kuliambia, na kutoa ulimwengu wote na mambo ya ulimwengu, na hivyo basi uamsho unaanza. Na ndipo yote yanapotulia, Kanisa liko katika hali nzuri basi, kuanza mwendo kisha kupokea karama za kiroho na baraka kutoka kwa Mungu, na hizo ndizo tunazotaka.

²¹ Siamini ya kwamba uamsho tunaotarajia kuja unakuja jinsi tunavyoutarajia, daima huja kinyume na kile tunachotarajia, Kristo alikuja tofauti, Yohana Mbatizaji.

²² Vema, kama mtu yeyote angaliwazia. . .Nadhani kama baadhi ya wafasiri wa Maandiko katika siku za Yohana wangesema, “Sauti ya mtu aliaye nyikani, itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito yake,” ninawazia baadhi yao walidhani ya kwamba Mungu angeshusha ushoroba kutoka

Mbinguni, kisha awe na gwaride la Malaika likishuka chini ardhini, ndipo nabii fulani mkuu, mwenye heshima angekuja akitembea kutoka Utukufuni.

²³ Nayo ilikuwa iwe kubwa sana, mpaka mabonde yote yatainuliwa, na mahali pote palipoinuka patashushwa chini, nayo milima ilikuwa iruke kama kondoo dume wadogo, na majani yote yatapiga makofi yao. Hilo lilikuwa liwe tukio la jinsi gani! Yale ambayo hapana shaka watu walitarajia kuona katika nyakati hizo!

²⁴ Lakini lilitukiaje? Maskini mhubiri aliyejaa mandevu huku amejizungushia ngozi ya kondoo, labda kamwe hakuoga kila baada ya miezi mitatu au minne, akajitokeza nyikani, amesimama kwenye matope kufikia magotini mwake, na kupaza sauti, “Tubuni, kwa maana Ufalme wa Mbinguni umekaribia!” Hapo ndipo mahali palipoinuka paliposhushwa, na mabonde yakainuliwa.

²⁵ Kile mwanadamu anachoita *kikuu*, Mungu hukiita *kipumbavu*. Na kile mwanadamu anachokiita *kipumbavu*, Mungu hukiita *kikuu*. Kwa hiyo kile tunachopaswa kufanya ni kurudi katika mpango wa Mungu na kuona, hata hivyo, kile Mungu anachotaka tufanye, na njia pekee nijuayo kufanya hivyo ni maombi; maombi ndiyo ufunguo, hilo ndilo jibu, maombi hubadilisha mambo.

²⁶ Maombi ndiyo silaha yenye nguvu kuliko zote iliyowahi kuwekwa katika—katika udhibiti wa wanadamu, hakuna bomu la atomiki, wala bomu la haidrojeni lenye nguvu kama maombi. Maombi yatabadilisha nia ya Mungu. Mlijua hilo? Yalifanya hivyo wakati mmoja.

²⁷ Nabii alitumwa kwa mfalme chumbani, na kusema, “Panda ukamwambie, BWANA ASEMA HIVI, yeye hatoki kitandani, atakufia papo hapo alipo.” Ndipo Isaya akakwea na kumwambia Hezekia jambo hilo.

²⁸ Nami naweza kuwawazia wa—watu mashuhuri wote wakiwa langoni, wakulima huko nje kwenye nyua za nje, walipoingia, kasema, “Loo, nabii wa Mungu, itakuwaje kwa mfalme wetu?”

“BWANA ASEMA HIVI, atakufa.”

Akatoka akaenda kwa askari, “Loo, nabii mkuu, Bwana anasema nini juu ya mfalme wetu?”

²⁹ “BWANA ASEMA HIVI, atakufa.” Na hiyo ilikuwa ni kweli, Bwana alimwambia hivyo. Anashuka, anaingia kwenye kibanda chake kidogo mahali fulani, huko nyuma nyikani.

³⁰ Ndipo Hezekia akaelekeza uso wake ukutani na kulia kwa uchungu, na kusema, “Bwana Mungu, nakuomba unifikirie, ninatembea mbele Zako kwa moyo mkamilifu. Ninahitaji miaka kumi na mitano zaidi kuuweka ufalme wangu katika hali nzuri.”

³¹ Na, mwajua, inaonekana kana kwamba endapo Mungu angetaka kusema lolote, angemwambia wakati alipokuwa akizungumza Naye, bali Mungu ana njia za kufanya mambo. Huna budi kuja kwenye njia za Mungu na njia za Mungu za kufanya mambo. Maadamu tunajaribu kujiingiza wenyewe, basi haitafaa kitu. Wala hatuwezi kujilinganisha sisi kwa sisi, hatuna budi kuishi kibinafsi mbele za Mungu.

³² Sasa, mtu aliye mkuu kuliko wote nchini, bila shaka, alikuwa ni mfalme; Mtu aliye mkuu kuliko wote Mbinguni alikuwa ni Mungu. Huyu hapo mtu aliye mkuu kuliko wote duniani, akizungumza na Mtu aliye mkuu kuliko wote Mbinguni, aliye mkuu kuliko wote Mbinguni, na hata hivyo yale mamlaka makuu ya Mbinguni hayangeweza kumjibu mfalme, kwa sababu haikukusudiwa kuwa hivyo, alikuwa ni mfalme tu. Ndipo basi akazungumza na Isaya, huyo alikuwa ni nabii Wake, na kusema, “Nenda ukamwambie ya kwamba nimeyasikia maombi yake, nami nitamwongezea hiyo miaka kumi na mitano.”

³³ Sasa, mnafikiri huyo nabii hapana shaka alitahayarikaje aliporudi moja kwa moja, “Kwa nini unarudi, Nabii?”

³⁴ “BWANA ASEMA HIVI, ataishi.” Huku ndio kwanza aondoke langoni akisema, “BWANA ASEMA HIVI, atakufa.” Akarudi, “BWANA ASEMA HIVI, ataishi. BWANA ASEMA HIVI, ataishi.” Kwa nini? Ni kitu gani kilichobadilisha? Maombi, hiyo ndiyo siri.

³⁵ Maombi hufungua mlango, maombi. “Lolote mtakaloomba katika maombi kwa imani mkiamini, mtapokea. Ombeni kwa wingi ili furaha yenu iwe timilifu.”

³⁶ Hebu na tumwombe Mungu, usiku wa leo, asiachilie chochote, bali amiminie nguvu za Mbinguni, kama itambidi kututikisa na kuturarua vipandevipande, na kushuka kwenda nyumbani kwa Mfinyanzi, na kufinyangwa tena, kama hilo ndilo linalohitajika, hilo ndilo ninalotaka. Nami nafikiri hivyo ndivyo kila mwaminio mwenye moyo mwaminifu anavyotaka, haidhuru inagharimu nini.

³⁷ Sasa, hebu na tukumbuke hilo wakati mkutano ukiendelea, “Sijali, Bwana, itagharimu nini, bali nataka Wewe unihuishe. Kama ni jambo ninalofanya, jambo ambalo sipaswi kufanya, jambo ambalo nilipaswa kufanya, nirarue tu vipande-vipande na unifinyange tena ili nikutii Wewe.” Nikiwa na kusudi hilo moyoni, Mungu ana hakika tu kujitokeza jukwaani, kama ninavyosimama nyuma ya mimbara hii. Hiyo ni kweli.

³⁸ Sasa, hii ndiyo mara ya kwanza ninayoweza kukumbuka katika historia yote ya mikutano yangu, ambapo nimewahi kufikia kiwango cha kufanya uamsho, sio ibada ya uponyaji. Nami nina furaha sana kwamba jambo hili limepangwa hivi. Nilifikiri kwamba labda ingekuwa, tungeenda huko Los Angeles, na hapa siku chache usiku, na huko juu, na namna

hiyo, bali ilitokea kwa namna fulani, ama ilipangwa katika uchumi mkuu wa Mungu kwamba nilikuwa niwe hapa, nadhani, kwa majuma haya mawili kanisani, nikifanya uamsho, kwa hiyo labda hivyo ndivyo Mungu anavyolitaka hilo, kwa hiyo tutamwachia tu. Yeye ndiye Bosi, sivyo?

Ni wangapi wanaompenda? Loo, ninyi ni, loo, hilo ni jema, basi inaonekana kana kwamba ni waaminio wote, hilo ni jema.

³⁹ Vema, hebu—hebu tuzungumze usiku wa leo, na kuitayarisha mioyo yetu kwa ajili ya ibada ya uponyaji kesho usiku. Halafu mnamo—mnamo Alhamisi usiku, tutaanza moja kwa moja na mafungu ya kiinjilisti, na kadhalika, Bwana akipenda. Na kuomba ya kwamba Mungu atatuweka katika uamsho kama huo ifikapo Jumapili, utukufu wa Mungu utakuwa unatunyeshea kila mahali, naye Mungu atakuwa akitenda kazi miongoni mwetu kwa maajabu makubwa na ishara, na mamia wakimpokea Roho Mtakatifu, na—na kwenda tu kila mahali.

⁴⁰ Sasa, hatuninii—hatumaanishi kusema sasa... Uamsho mkuu wa kweli, haupewi kichwa cha habari, na mambo kama hayo. La, la. Kuna jambo moja ambalo Yesu Kristo alikosa maishani Mwake, nachukia kusema hilo, bali alilikosa, Yesu alipungukiwa na kitu kimoja, maonyesho mamboleo, Yeye hakuwa mtu wa kujionyesha, la. Yeye... wao... Kila mtu, leo, hana budi kuwa na vichwa vikubwa vya habari, na kujigamba kwa yale wanayofanya, hayo ni majivuno. Hiyo ni kweli. Huyu si mtumishi wa Mungu, mtumishi wa Mungu atakuwa mnyenyekevu, akijizua.

⁴¹ Na wakati uamsho ujapo, angalieni kile ambacho kimekuja daima, kilipokuja katika siku za Yesu, katika uchache tu, watu wachache tu. Angalieni kile Yohana alichokuwa nacho huko ufukoni, watu wachache tu walikusanyika, kutoka maeneo ya karibu, kumsikiliza. Yapata asilimia tisini na tisa yao waliukataa Ujumbe wake na kuondoka, hata hivyo ulikuwa ni uamsho mkuu, na wakati wa kutikisa.

⁴² Mungu huvitikisa vitu, nao watu hawatambui inatendeka. Mnaona, Mungu hulitikisa Kanisa Lake, uamsho ni kwa Kanisa Lake. Ninaamini Kanisa limeitwa litoke sasa, lakini jambo la kuamsha, ni kuliambsha na kulitikisa Kanisa hilo lirudi mahali Pake tena.

⁴³ Mtu fulani alisema, “Kwa nini unajipumbaza na kundi la Wapentekoste, watakatifu wanaojibingirisha, na kadhalika?” Vema, huko ndiko nilikotumwa, mimi ni mmoja wao. Kwa hiyo wao—wao wanasema, “Mbona wewe, unafanya ishara hizi, kwa nini usiende mahali pakubwa, mahali pa juu, na kadhalika?”

⁴⁴ Kama ukiangalia, hilo ndilo jambo lile lile lililosemwa kwa Bwana wetu. Ndugu Zake hata walimwambia, “Kwa nini usije mbele ya Kayafa, ama baadhi ya ma—mahali pakubwa na

ujionyeshe? Ikiwa wewe, ukiwa ndiwe Jamaa huyu, Kristo huyu, acha wajue wewe ni nani.”

⁴⁵ Akasema, “Siku yenu ni sikuzote.” Yeye hakupanda kwenda pamoja nao, lakini saa Yake ilikuwa bado inakuja; Yeye hakuwa mtu wa maonyesho. Nami nafikiri hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, linajionyesha kupita kiasi badala ya kuwa na Kristo wa kutosha. Mnaona? Tunamtaka Kristo, si maonyesho, Kristo, tunataka kuiandaa mioyo yetu. Ndipo tutakapofikia mahali hapo, mtaona ya kwamba Mungu ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye hashindwi.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu, na kumwendea Mwandishi, kabla hatujalikaribia Neno Lake.

⁴⁶ Baba yetu wa Mbinguni, kwa kweli sisi ni watu waliojaliwa, usiku wa leo, kukusanyika pamoja hapa katika taifa huru, ambapo tunaweza kumwabudu Mungu kwa mwongozo wa dhamiri zetu. Tuna furaha sana kwa ajili ya jambo hili, na kwa ajili ya mlango ambao bado umefunguliwa, katika nchi yetu, tukijua ya kwamba haitachukua muda mrefu sana sasa, mpaka fursa hizi zitakapoondolewa kwetu. Na, Bwana, litakuwa ni jambo kuu wakati litakapotukia, kwa sababu basi upendo wa Mungu utatushurutisha, mpaka mioyo yetu itaungana pamoja.

⁴⁷ Ninaomba, Baba, kwa ajili ya mkutano huu ujao, kwa ajili ya Long Beach, na kwa ajili ya kanisa hili, lililoitwa kwa kusanyiko la Mungu, na ambapo watoto wa Mungu wanakusanyika, pamoja. Nalo kanisa ni watu wanaoufanyiza mwili.

⁴⁸ Nasi tunaomba, Mungu, kwa ajili ya mchungaji huyu, ninaomba ya kwamba utambariki, Bwana. Na kwa kuifungua mikono yake, na moyo wake, kwa ajili ya uamsho kuanza, maombi yao na yasiwe ya bure, bali naomba Wewe utujibu juma hili kwa uamsho mkuu ambao utashika moto kote juu na chini ya Pwani hii ya Magharibi, Bwana.

⁴⁹ Nao watu wa Mungu watambue ya kwamba kama ilivyokuwa katika wakati wa Ezekieli, mifupa iliendea mifupa na ngozi juu yake, nao wakasimama, lakini hata hivyo ilihitaji kutabiriwa, kuufanya uhai uingie ndani yake.

⁵⁰ Na Baba wa Mbinguni, huenda tukaunda madhehebu, na kuyakusanya makanisa pamoja, na—na kuunganisha mikono yetu, na kwenda mfupa kwa mfupa, lakini hata hivyo inahitaji unabii wa upepo unaotikisa kuturudishia uhai tena. Baba, tunaomba ya kwamba hakutakuwako tu na m—mkutano wa muda mrefu, bali uamsho ambao kweli utatikisa kila moyo, kila nyumba, kila kanisa, kila mshiriki, mpaka Roho Mtakatifu atakapokuwa ametawala katika kila maisha.

⁵¹ Kutoka hapo, Bwana, watenda kazi watatoka waende kwenye kona za barabara na vijia, bila mwonekano wa aibu usoni mwao, bali kama askari hodari wakiwaka moto, nyuso kama ule wa Stefano ulivyokuwa, wakati, kama nyumba

inayoungua moto katika upepo mkali, wasingeweza kumzuia, wala lile Baraza la Wazee lisingeweza kumzuia, bali aliwapigia kelele, “Wenye shingo ngumu, wasiotahiriwa mioyo wala masikio!”

⁵² Hata mauti yenyewe hayakuukomesha Ujumbe wake, ulimfikia Sauli wa Tarso, kamwe haukumwacha mpaka, Mungu, Wewe ulipomtia moto na kumwanzisha, ndipo akawa mtume kwa wakati wa Mataifa.

⁵³ Mtu huyo mmoja, wakati alipokuwa anakufa, amepiga magoti yake, na kusema, “Ninamwona Yesu amesimama mkono wa kuume wa Mungu,” *mtazamo* huo wake!

⁵⁴ Mungu, tunaomba ya kwamba utamtuma Roho Mtakatifu katika nguvu kuu sana za kushawishi ambaye ataweka *mtazamo* huo wa azimio juu ya kila moyo na juu ya kila uso unaokusanyika katika kanisa hili. Tujalie, Bwana, kwamba huenda kukawa na wakati wa kuchunguza nafsi, kwa kuwa tunatambua kwamba tunaishi katika saa iliyochelewa, iliyochelewa kuliko tunavyowazia. Ulisema ungekuja katika saa usiyodhania, kwa hiyo huenda ikawa ni wakati wowote.

⁵⁵ Ninaomba, Baba, ya kwamba utanisaidia, nikizungumza dakika chache zilizopita, juu ya kusema wale wapanda farasi wanne, uponyaji wa Kiungu, chochote kinachoweza kuanguka, Bwana, tunakufungulia tu mioyo yetu, Wewe njoo, utushughulikie, Bwana, kulingana tu na haja tuliyo nayo. Ukutilie mbali ulimwengu wote kutoka kwetu, Bwana, chukua Upanga Wako mkali, wenye makali kuwili, Neno, na kuyatambua mawazo ya mioyo yetu na nia, na kutukumbusha mahali ambapo tumepungukiwa. Na jalia tusiache kuomba, mpaka tutakapoona maombi yetu yakijibiwa. Tujalie, Baba.

⁵⁶ Itahiri midomo yangu, itahiri mioyo ya hawa watu, ili niweze kunena nao waweze kulisikia Neno la Bwana. Tunaomba haya kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Jina la Mwanawe, Yesu Kristo. Amina.

⁵⁷ Ninamwomba Bwana Yesu, ya kwamba uamsho utanza tangu sasa na kuendelea, ambapo kila mtu, anaona njaa na kiu. Sasa, jiandaeni tu, kila mtu, usimngojee jirani, si kitu juu ya jirani, sisi wenyewe. Hebu na tufunge, tuombe, tumwite Mungu, tupige simu, tumwite mtu fulani, tuwalete huku, tuwaongoze watoto wetu kwenye maombi, tuyakusanye makundi ya familia zetu pamoja, tuifungue tu mioyo yetu, na kusema, “Bwana, sisi hapa.”

⁵⁸ Sasa, juu ya kujiandaa kwa ajili ya ibada kesho usiku kwa ajili ya ibada ya uponyaji basi, hao wavulana watakuwa hapa na kadi za maombi yapata saa kumi na mbili u nusu, ninyi mnaotaka kadi za maombi, njoni. Na hebu wagonjwa waje wanizunguke, hapa juu, wengi wenu mmekuwa kwenye mikutano, nanyi mnajua jinsi inavyofanya kazi.

⁵⁹ Ningeninii. . . Ni afadhali mtu kuketi hapa mwenye imani akiamini, akiketi mbele, kuliko huko nyuma, kwa sababu wakati mwingine ninapowaona huko nyuma, mimi . . . kuna wengi sana kati ya hao, wakati hiyo, ambapo *mifereji*, ninaiita, ama—ama, miale ya imani inayotoka kwa watu, inatatanisha, hata hivyo, inaenda kote kwenye umati, na maelfu mara maelfu ya watu, lakini afadhali niwalete wagonjwa hapa mbele, karibu na mahali nilipo.

⁶⁰ Sasa, usiku wa leo, ninataka kuzungumza juu ya somo, kwanza, ninataka kuwasomea kifungu kutoka katika Maandiko, kinachopatikana katika Luka Mtakatifu mlango wa pili, kifungu cha 26:

Na tazama, huko Yerusalemu palikuwa na mtu, jina lake Simeoni; . . . mtu huyo mwenye haki, mcha Mungu, akiitarajia faraja ya Israeli, na Roho Mtakatifu alikuwa juu yake.

Naye alikuwa ameonywa na Roho Mtakatifu, ya kwamba hataona mauti, kabla ya kumwona Kristo wa Bwana.

⁶¹ Sasa, ninataka kuchukua somo la *Tarajio*. Sasa, kabla hujaweza kuwa na tarajio, lazima kuwe na imani ya kuambatana na tarajio hilo. Na kuna elementi mbili tu ulimwenguni zinazoutawala ulimwengu, usiku wa leo, ambazo ni hofu na imani. Urusi inajaribu kumfanya kila mtu awaogope, nasi tunajaribu kumfanya kila mtu kumwamini Mungu, sasa, hiyo ndiyo tofauti. Elementi hizo mbili zinatawala mataifa yote, zinawatawala watu wote, zinatawala makanisa yote, zinawatawala watu binafsi, ni hofu ama imani.

⁶² Sasa, hofu haina thamani ndani yake, hata kidogo, haina mwisho kabisa, haina, haina jambo moja jema kwake. Kama nilikuwa nipigwe risasi asubuhi, nilikuwa nipigwe risasi, ingefaidi nini kuwa na hofu? Ingenifaidi nini?

Unasema, “Vema, imani itakufaidi nini?”

⁶³ Imani ingeweza kunikomboa, bali hofu haitanisaidia hata kidogo. Unajichochea sana, na kushikwa na wasiwasi zaidi inapofikia wakati wa bunduki kufyatuliwa. Kwa hiyo, hebu na tuwe na imani. Imani ingeweza kunikomboa, lakini kama hainikomboi, hofu ingefaidi nini, kwa vyovyote vile? Dumu tu moja kwa moja na imani, na uishikilie. Chukua ahadi ya Mungu na ubaki na Mungu.

⁶⁴ Na sasa, tunapoanza kusoma Neno na kufundisha Neno, kamwe sitatoka nje ya Neno kwa ajili ya chochote, na ukumbuke, ya kwamba huna budi kuamini jambo hili katika Mungu: kwamba Mungu hutimiza Neno Lake. Atafanya hivyo, asipofanya hivyo, Yeye si Mungu. Yeye ni, Mungu hana kikomo, na wakati kitu chochote hakina kikomo, ni, vema, hakuna njia ya kuelezea kisicho na kikomo ni nini.

⁶⁵ Lakini sisi tuna kikomo, kwa hiyo tunaweza kusema lolote, na kesho yake, ama saa moja kutoka hapo, ama dakika tano itatubidi kulibadilisha, na kusema, “Loo, nilikosea.” Lakini Mungu hawezi kufanya hivyo kama Yeye hana kikomo. Kwa sababu Yeye hufanya ninii Yake—Yeye hufanya ahadi Ya—Ya—Yake, wala kamwe hawezi kuighairi. Ahadi Yake daima ni bora kuliko zote, uamuzi Wake daima ni mkamilifu. Na kama ni mkamilifu, kamwe hauwezi kuwa mkamilifu *zaidi*, kwa hiyo sikuzote hauna budi kuwa sahihi. Sasa, basi kama una imani . . .

⁶⁶ Nilikuwa nikizungumza na da—daktari fulani wakati fulani uliopita kuhusu mmoja wa wagonjwa wake aliyekuwa ameponywa, akasema, “Mbona, Billy,” yeye ni rafiki yangu, akasema, “hakuna—hakuna shaka hata kidogo,” kasema, “jamani, kansa ilikuwako.” Kasema, “Nilimfanyia huyo mtu upasuaji, wala sikuweza kuipata, ilikuwa kooni mwake.” Naye akasema, naye alikuwa shemeji wa daktari, ndipo akasema, “Imekwisha kabisa.”

⁶⁷ Na baadhi ya watu walikuwa huko nje kwa mtu aliyesimamia hiyo moteli, tulipokuwa tukifanya mkutano, alikuwa akimwambia kila mtu habari zake, na jinsi ambavyo kwamba imani ililifanya, akasema, “Naam, Billy, ninaamini hilo.” Kasema, “Sasa, kuamini,” kasema, “sasa, naamini kama angalitoka akaenda na kugusa mti na kusema aliamini . . .”

Nikasema, “La, hilo halitafanya kazi.”

Akasema, “Kama aliamini.”

Nikasema, “Hana msingi wowote wa imani.”

⁶⁸ Kugusa mti ukiamini, huo ni ushirikina, huna budi kuwa na msingi wa imani. “Nayo imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu.” Sasa, kabla . . . Ukiichukua tu kama ripoti yoyote ya gazeti, ama chochote kile, mbona, huwezi kuamini jambo hilo, watakosea kwa sababu wao ni wanadamu, bali Biblia hii haiwezi kukosea, haina budi kuwa kamilifu kwa sababu ni Neno la Mungu.

⁶⁹ Wala Mungu si bora kuliko Neno Lake, ama wewe si bora kuliko neno lako, mimi si bora kuliko neno langu. Kwa hiyo, basi wakati Biblia inaposema jambo lolote, kumbukeni, latosha milele.

⁷⁰ Na kama Mungu akiwahi kuitwa jukwaani kufanya uamuzi juu ya jambo fulani, nao uamuzi aliofanya wakati alipoitwa jukwaani kwa ajili ya jambo lile lile tena, uamuzi Wake hauna budi kubaki vivyo hivyo. Hawezi kuubadilisha kwa mmoja, akisema, “Vema, nilimfanyia *huyu*, na, lakini sitamfanyia *huyu*.” Sasa, kama akifanya hivyo, basi alifanya uamuzi mbaya alipoufanya mara ya kwanza. Kwa hiyo, Yeye amelifanya Neno Lake hivi kwamba “Kama mnaweza kuamini . . .”

⁷¹ Wakati yeye, mtu fulani alipomwomba msamaha wa dhambi zake, na Mungu akamsamehe mtu huyo dhambi zake, kama ukija, ama yeyote atakayekuja juu ya msingi ule ule wa kuomba msamaha kwa unyenyekevu, kwa msingi wa imani, Mungu anawajibika kufanya jambo lile lile alilomfanyia mtu huyo mara ya kwanza.

⁷² Na kama mtu kamwe akiwa mgonjwa na kumwita Mungu, na kama Mungu akimponya mtu mmoja, aliwahi kumponya mtu mmoja, na kwa misingi ile ile aliyomleta mtu huyo kwa ajili ya uponyaji wake, kama akipata kuitwa tena, hana budi kubaki na uamuzi ule ule. Kama hakufanya hivyo, alifanya kosa, halafu kama alifanya kosa, Yeye si asiye na kikomo, na kama Yeye—kama Yeye si asiye na kikomo, basi Yeye si Mungu.

⁷³ Unaona, huna budi kurudi moja kwa moja kujua Neno hili ni kweli. Sasa, hilo ndilo hasa linalonipa msimamo wangu jasiri katika Kristo, kwa sababu ninaamini Neno hilo ni kweli. Kamwe haliwezi kushindwa, haliwezi kushindwa si zaidi ya Mungu, kwa sababu ni Mungu, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.”

⁷⁴ Waebrania 4 inatwambia ya kwamba Neno la Mungu lina nguvu, lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, ukikatilia mbali pande zote mbili na mafuta ya mfupa, na hata ni Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo. Wakati Yesu alipowaangalia wasikilizaji na kutambua wazo lao, ilikuwa ni nini? Yeye alikuwa ni Neno, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.” Vema, walipaswa kujua jambo hilo, ya kwamba Yeye alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Sasa, Neno lilo hilo la Mungu lililonenwa, Roho Mtakatifu, anaweza kufanya ahadi yoyote ya Mungu idhihirike, kama tu utaamini.

⁷⁵ Sasa, matarajio, hayana budi kujengwa juu ya kitu kilicho na imani nyuma yake, kwa sababu kama unatarajia jambo fulani ni kwa sababu jambo fulani limeahidiwa ama njia fulani namna hiyo. Kwa hiyo ukitaka kuwa na matarajio halisi lazima yajengwe juu ya BWANA ASEMA HIVI.

Mwangalie Nuhu, ilikuwa...wakati mwingine Mungu alikuagiza ufanye mambo ambayo ni ya dhahaka kwa mawazo yako ya kibinadamu.

⁷⁶ Sasa, kumbukeni, kama utaingia kwenye uamsho huu ukijaribu kuwazia jambo fulani, kwanza kabisa afadhali uondoke, maana huwezi kufanya hivyo. Kumbuka, Mungu hamjui mwanadamu kwa, ama mwanadamu hamjui Mungu, hasa, kwa kichwa chake, anamjua kwa moyo wake. Katika bustani ya Edeni, mtu aligawanywa kati ya Mungu na Shetani; Shetani alichukua kichwa chake, Mungu akautwaa moyo wake.

⁷⁷ Kwa akili zake, anajaribu kuhoji mambo, bali kwa imani moyoni mwake, kwa njia ya Mungu, itamfanya aamini mambo ambayo hoja hata haitathibitisha, “Kwa maana ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.” Mnaona, hana budi kuliadini Neno la Mungu. Loo, ndugu, laiti ungaliweza tu kupata hilo vizuri na kulizamisha moyoni mwako, ingemfanya kila ibilisi aruke na kuondoka, sasa hivi. Unaona? Kujua! Hu—hufanya hivyo.

⁷⁸ Sasa, ni—ni—ninajua ninalozungumzia, nimekuwa, hii ni miaka thelathini na moja katika huduma kwangu, nami ni—ninajua ninalozungumzia. Nami sijawahi, kwa uaminifu, maishani mwangu mwote, kumwomba Mungu chochote, huku Biblia hii imefunguliwa, pasipo Yeye kunipa, ama kuniambia ni kwa nini asingeweza kufanya hivyo. Na hiyo ni kweli. Maana kuna wakati mwingine Yeye hawezi kunipa, maana nafikiri ninataka, na Yeye anajua vema zaidi, lakini Yeye daima amekuja na kuniambia ni kwa nini. Na kwa hiyo na—najua hiyo ni kweli. Kwa hiyo, Mungu hutimiza Neno Lake, unaweza tu kutegemea hilo.

⁷⁹ Sasa, Nuhu alipoambiwa na Mungu ajenge safina, kwa nini alihofu, akijua...Ungeweza kuwazia yale wakosoaji waliyokuwa wakisema? Nuhu alikuwa akitarajia kunyeshe, kwa sababu Mungu alisema itanyesha. Sasa, kamwe haikuwa imenyeshajuu ya nchi, ungeweza kuwazia wakosoaji wakisema, “Loo, angalieni, maskini, jamaa mzee kidogo amerukwa na akili.” Lakini akasema...“Mvua hiyo iko wapi Nuhu? Niambieni iko wapi, sioni yoyote yake huko juu, ha—hakuna mvua kutoka huko juu, haijawahi kuwa, haitakuwapo kamwe.”

⁸⁰ Lakini Nuhu akasema, “Mungu alisema hivyo, hilo latosha. Kama Mungu alisema hivyo, Yeye anaweza kuumba mvua huko juu kama alitaka.” Kwa hiyo, alikuwa akitarajia inyeshe, kwa hiyo akafanya maandalizi kwa ajili ya mvua.

⁸¹ Loo, napenda hilo. Loo, fanya maandalizi maadamu unalisikia Neno la Mungu, basi fanya maandalizi kwa ajili ya jambo hilo kutukia, na ungojee chini ya matarajio. Loo, kwanza kabisa hilo linanifanya nianze kujisikia kubarikiwa. Mnaona? Kuwazia ya kwamba Mungu alisema hivyo, kisha kufanya, kuwa ukilitarajia.

⁸² Sasa, kama Mungu ameahidi uamsho hapa, tutaupata, hebu tujiandae kwa ajili yake. Kama Mungu aliahidi kuponya, hebu tujiandae kwa ajili yake. Yesu alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya,” hebu tujiweke tayari kwa ajili yake, tuondoe kila kitu, tuwe tayari. Tuko katika wakati mzuri. Kwa hiyo ninii tu... .

Sasa, itaonekana ni upumbavu. Sasa, unasema, “Vema, itatendekaje katika siku kama hii, na wakati haya yote...?”

⁸³ Sijali ni kitu gani kinyume na hilo, ni—ni makosa. Hatuwezi kuliona, sioni tumaini lake, inaonekana, lakini kama Mungu alisema hivyo, hebu na tulifanye kwa vyovyote vile, maana Mungu alisema hivyo. Itatendeka kwa vyovyote vile, ni—ninalitarajia.

⁸⁴ Ninaamini Yesu yuaja. Sayansi inathibitisha wanaweza kuchukua chavua kidogo kutoka kwa *kitu kingine*, na golegole kidogo, na kuweka kitu ndani yake, na kadhalika namna hii, na karibu wanaweza kufanya uhai wa binadamu, wanadai. Loo, wao ni werevu sana wanaweza, wana sputniki huko juu angani, na moyo wa mwanadamu ukidunda ndani yake, hilo halinisumbui hata kidogo.

⁸⁵ Wanasema, “Loo, moja ya siku hizi utaona kwamba dini yote unayozungumzia ni wazimu.”

⁸⁶ La, sivyo, Yesu atakuwa hapa, tutakuwa na Utawala wa Miaka Elfu, tutaenda Nyumbani Utukufuni, ninatarajia hilo, kwa hiyo ninafanya maandalizi kwa ajili yake, ninakungojea, kila siku nikiwa tayari. “Atakuja lini?” Sijui, lakini kama Yeye hayupo hapa leo, nitakuwa nikiangalia kesho. Ninautarajia, kwa sababu tu Yeye alisema hivyo, nami ninaishi kila siku chini ya matarajio hayo. Hiyo ni kweli. Lazima tuwe na matarajio, bila shaka.

⁸⁷ Nuhu, uh, Ibrahimu, mbona, wakati aliposikia Neno la Mungu, naye akashuka katika nchi ya Ukaldayo katika mji wa Uru, akishuka kutoka Shinari, labda, kutoka labda kwenye familia ya kikafiri huko juu ni juavyo mimi, lakini siku moja, tuseme alikuwa ni mkulima huko shambani, kisha Mungu akasema naye, alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano, mke wake alikuwa na sitini na mitano, Naye akasema, “Ibrahimu, utampata mtoto kwa mkeo, Sara,” vema, alitoka akaenda akafanya maandalizi yote. Kwa nini? Alikuwa akimtarajia. Alikuwa akimtarajia huyo mtoto kuja, wakati wowote.

“Je, itakuwa ni siku ishirini na nane zijazo, utajua habari zake?”

“Sijui. Kama sivyo, labda hizo ishirini na nane zijazo.”

⁸⁸ Mara ya kwanza, ninawazia, alimwambia Sara, “Unajisikiaje, Mpenzi?” baada ya mwezi wa kwanza kupita.

“Hakuna tofauti.”

⁸⁹ “Mungu ashukuriwe, tutampata, kwa vyovyote vile. Endelea na kutengeneza vijibuti, na utayarishe lile koti dogo, chukua macho-ndege yote na pini, maana tutampata. Hiyo ni kweli. Ninamtarajia. Hiyo ni kweli. Ziweke kwenye sanduku lako la matumaini, ukajiandae kwa sababu yuaja.”

Mwaka mmoja ukapita, “Tofauti yoyote, Mpenzi?”

“Hata kidogo.”

“Tutampata, kwa vyovyote vile. Ninamtarajia.”

⁹⁰ Mungu alisema, “Jitenge na jamaa yako.” Hilo ndilo unalopaswa kufanya mara nyingi, kujitenga na kutokuamini kwingi. Basi kumbukeni, mpaka Ibrahimu alipomtii Mungu kikamilifu, ile baraka haikuja, mpaka alipomtii Mungu kikamilifu. Aliondoka na baba yake, naye akasababisha matatizo, kisha hatimaye Lutu akasababisha matatizo, na mchungaji, na ndipo mara alipojitenga na kila kitu, kama vile Mungu . . . alipotii kikamilifu, alipofikia utiifu mkamilifu, ndipo Mungu akaleta baraka.

⁹¹ Sasa, kanisa la Kipentekoste limekuwa likitarajia ku—kuzuriwa kwenye Nchi ya Ahadi kwa ajili ya kurudishwa kwote kwa karama na kadhalika. Lakini mara ilipoanza kunena kwa lugha na kufasiri, ndipo wakaanza kuunda madhehebu, kuunda madhehebu mbalimbali, wakijitenga, na mambo kama hayo, mmepigana kwa muda wa miaka arobaini, mtaendelea tu kupigana maadamu mnafanya hivyo.

⁹² Lakini mnapokusanyika pamoja, kama walivyofanya kwenye Siku ya Pentekoste, kukusanyika, basi mtarajie Mungu kufanya jambo fulani. “Ikiwa watu walioitwa kwa Jina Langu watakusanyika pamoja na kuomba, basi nitasikia kutoka Mbinguni.” Sasa, kama tutafanya hivyo, tunaweza kutarajia jambo fulani, mpaka tutakapofanya hivyo, afadhali tusilitazamie, kwa sababu haliji. Hatuna budi kumtii Mungu kikamilifu.

⁹³ Huna budi kufikia mahali ambapo A—Assemblies of God, na Church of God, na Foursquare Church of God, na Umoja, na Uwili, na Utatu, na Utano, na maskini hizo *itikadi* zingine zote ndogo mlizojitenga kwazo, mtasahau tofauti zenu, na kukusanyika na kuomba, basi nitatarajia kusikia kitu kutoka Mbinguni.

Ninyi . . . Loo, wanasema “Vema, watafanya *hivi*.”

⁹⁴ Vema, hivi majuzi shirika fulani, nilipokuwa Beaumont, Texas, kwa sababu nilikuwa nimeketi jukwaani, kutoka (Kanisa moja lilionidhamini.) yapata makanisa arobaini na mawili, nao wote walikuwa watu wazuri, ndipo mzee wa wilaya akanipigia simu, na kusema, “Ninachora mstari, tangu sasa na kuendelea, Bw. Branham, ninakuchora utoke, ulikuwa na mtu aliyeketi jukwaani aliyebatizwa vibaya.”

⁹⁵ Vema, nikasema, “Nitafanya jambo tofauti na hilo, nitachora mstari mwingine, nikuingize ndani. Ukinitoa nje kwa mmoja, nitachora mwingine, nikurudishe ndani.” Hiyo ni kweli.

⁹⁶ Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo, tutandaze mahema yetu, huko mbali sana, tupate kila ndugu, naam, bwana, hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya. Ndipo basi tunapofanya hivyo, tunaweza kumtarajia Mungu kujibu, lakini mpaka tutakapofanya hivyo,

Yeye hatajibu, kwa sababu hatuna budi kujitenga na mambo ya ulimwengu.

⁹⁷ Na maadamu kanisa la Kipentekoste linaendelea kutamani mambo ya ulimwengu, na *hili*, *lile*, na *linginelo*, na, loo, afadhali hata uondoke. Mpaka utakaporudi kwenye Injili halisi tena, urudi kwenye Neno la Mungu, urudi kwenye BWANA ASEMA HIVI, hatutafanikiwa kamwe mpaka tutakapofanya hivyo, Mungu hatasikia, mpaka tutakapomtii Mungu kikamilifu. Naam, bwana.

⁹⁸ Wakati Ibrahimu alipomtii Mungu kikamilifu, basi alijua ya kwamba alipofanya hivyo kikamilifu, ndipo mara moja Malaika watatu wakaja, na kutangaza kuzaliwa kwa huyo mtoto mchanga, naye akaja. Lakini Ibrahimu hakukata tamaa, aliendelea tu kumtarajia, akaendelea kumtarajia, na hatimaye akajiingiza kabisa katika mapenzi ya Bwana, ndipo ikatukia, lakini mpaka atakapofanya hivyo, kamwe halitatendeka.

⁹⁹ Musa, inawafanya watu watende mambo ya kuchekeka wakati wao—wakati wanaposikia kutoka kwa Mungu wakati mwingine. Musa alikuwa mwanatheolojia mashuhuri, alifundishwa katika hekima yote ya Wamisri, mbona, bila shaka, hakuna kitu ambacho Musa hakujua.

¹⁰⁰ Sasa, sijui kama huko nyuma miaka arobaini jangwani, huku akiwachunga kondoo, vipi kama angaliwazia, “Ninaamini nitashuka nirudi Misri na—na niboreshe ninii yangu, loo, labda hisabati yangu kidogo,” mbona, alijua mengi sana angeweza kuwafundisha walimu, hakuhitaji elimu yoyote, haikumbidi kufundishwa chochote, kwa kuwa alijua yote, bali alishindwa kwa yote aliyojua.

¹⁰¹ Sasa, ninaamini katika shule za Biblia, ninaamini tunapaswa kufanya hivyo, tunapaswa kuwa na shule za Biblia. Mvulana wangu ndiyo kwanza atoke Waxahachie, nina msichana anayejiandaa kuingia mle, Shule ya Waxahachie ya Assembly of God, huko Waxahachie, Texas. Ninaamini hilo, lakini, ndugu, tunapoanza kufundisha katika, shule zetu na seminari, njia sahihi tu ya kuzungumza, na kadhalika, na yote, elimu, kadhalika, tunachohitaji, leo, katika seminari na kadhalika, ni kumrudia Mungu, kumrudia Mungu; si mipango yetu ya elimu, bali mpango wetu wa wokovu.

“Ati enendeni ulimwenguni kote, mkaunde seminari”?

La, bwana.

“Ati enendeni, ulimwenguni kote, mkajenge makanisa”?

La, bwana. Hayo ni sawa.

“Ati enendeni, mkajenge hospitali”?

¹⁰² La, bwana, hayo siyo yale Kanisa liliagizwa kufanya, makanisa yanajenga hospitali, makanisa yanajenga shule,

makanisa yanajenga majengo, lakini hili hapa agizo: “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili.”

¹⁰³ Injili ni nini? Si Neno tu, Paulo alisema, bali dhihirisho la Neno, “Injili ilitujia si katika Neno tu, bali kwa nguvu, na madhihirisho ya Roho Mtakatifu.” Kwa maneno mengine, “Enendeni ulimwenguni kote, mkaonyeshe nguvu za ufufuo. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Kufundisha tu Neno hakutafaa, huna budi kuwa na nguvu za Roho Mtakatifu nyuma ya hilo Neno kulifanya lipate Uzima tena. Amina. Litakuwa Hai.

Unasema, “Loo, Ndugu Branham, hiyo ilikuwa miaka elfu mbili iliyopita.”

¹⁰⁴ Vema, mkosoaji, ninataka kukufunga kinywa, sasa hivi. Unaona? Hapa si muda mrefu uliopita, ukiangalia kwenye gazeti la *Life*, walienda kwenye yale maghala makubwa ya Misri na kutoa baadhi ya hiyo ngano ambayo Yusufu aliweka mle, wakaipanda ardhini, nayo ikaota. Walipata (Ilikuwa ni nini?) mbegu ya alizeti, ama chochote kile, miaka elfu nne iliyopita, kutoka kwenye—kutoka kwenye kaburi la kale la Mfalme Tut, mbegu ya alizeti, na kuipanda, naye Mungu alikuwa ameuhifadhi uhai huo. Kabisa.

¹⁰⁵ “Ingawa mabuu ya ngozi yatauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu.” Neno la Mungu halitaangamizwa kamwe. Neno la Mungu, kama utalipanda katika mazingira mazuri juu ya Neno la Mungu, litafanya jambo lile lile lililofanya hapo mwanzo. Hiyo ni kweli, hiyo ni kweli.

¹⁰⁶ Wakati fulani uliopita nilikuwa nimeketi huko chini Kentucky, nikiwinda kuchakulo. Vema, mimi—mimi, hivyo ndivyo ninavyofanya kujiburudisha, ni—ninawinda, kupiga shabaha na kadhalika, kujipumbaza kwa bunduki, hiyo ni burudani tu. Nami nilikuwa na bunduki ndogo ya Winchester Muundo 75, kwenye yadi hamsini, nikasimama kwenye uwanja wa shabaha na kulenga shabaha tisa kikamilifu kwenye kijisumari cha zulia kwayo, moja kwa moja kupitia kwenye karatasi.

¹⁰⁷ Halafu basi, muda si muda mwajua, wakati ningempiga risasi yule kuchakulo, ingenibidi kuona pembe nne za jicho lake. Iwapo aniangalia, nisingempiga risasi, kama angekuwa amegeuza mgongo wake, nisingempiga risasi, ilimbidi kuketi vizuri. Yadi thelathini, ningeachana naye, yadi ishirini, ilibidi awe yadi hamsini. Hiyo tu ni kwa sababu nina ya kutosha namna hiyo.

¹⁰⁸ Siku moja hiyo bunduki ndogo iliharibika, nami nisingeweza kabisa kuitengeneza hata kidogo, niliikarabati, nami nikafanya kila kitu nilichoweza kufanya, na kuikaza, legev. Mtetemo wa moja kati ya elfu tano tu *hapa* utaiweka kombo nusu inchi kwenye yadi mia moja. Kwa hiyo, mnaona, wewe... Sehemu fulani imekaza, nyingine imelegea, huna budi kuiweka *sawa*.

¹⁰⁹ Kwa hiyo nikairudisha kwa Kampuni ya Winchester, nami ninayo hiyo barua nyumbani sasa, walisema, “Kasisi Branham, bunduki hiyo haina kasoro hata kidogo.” Kasema, “Bunduki hiyo itakosa shabaha kwa inchi moja kwenye yadi ishirini na tano, wala Muundo 75 haitakuwa bora zaidi.” Kasema, “Kwanza kabisa hiyo si bunduki ya kulenga shabaha.” Kasema, “Ina skrubu moja tu ya mguu inayoishikilia pamoja, kwa hiyo huna budi kupata mtetemo kutoka kwake.”

¹¹⁰ Sasa, huyo alikuwa ndiye mtu aliyetengeneza na kuifanya hiyo bunduki, Kampuni ya Winchester, yale mathibitisho, mtu aliyetumia maisha yake yote, na wahandisi, kutengeneza hiyo bunduki, walisema, “Haitaenda kombo zaidi ya inchi moja kwenye yadi ishirini na tano.” Nami nilikuwa nikilenga shabaha kwenye yadi hamsini nayo.

¹¹¹ Sasa, niliketi chini ya mti siku moja, huku nikilia tu. Kuna Ndugu Wood na marafiki zangu kadhaa huko juu wakiwapiga risasi kuchakulo, sikujali walimpiga wapi, kishindo tu, na mahali popote ilipompiga ni sawa, kwangu mimi, nilifikiri huenda nikashuka chini kwenye shavu lake, nimpige kidogo nyuma ya masikio, ama kitu fulani, hilo lisingekuwa sawa, ilibidi ilipige jicho, haikuwa sawa.

¹¹² Ndipo nikawazia, “Vema sasa, haileti tofauti yoyote yale Kampuni ya Winchester isemayo, ninajua ya kwamba itafanya hivyo kwa sababu nimeiona ikifanya.”

¹¹³ Nami nilikuwa nimeketi pale asubuhi moja chini ya maskini mti mdogo uliopinda, nikilia, nika—nikashikwa na wasiwasi sana nikaanza kulia, nikasema, “Bwana, mimi huyu hapa mbali na ibada, huku nje mwituni nikijaribu kupumzika. Na maskini mtu mwenye wasiwasi kama mimi, kwa nini kamwe ulijaribu kunituma nje mkutanoni, kwa vyovyote vile? Kwanza kabisa mimi nimeshindwa, na kwa nini ukamtuma mtu kama mimi kamwe? Ilionekana kana kwamba ungemchukua mtu ambaye alikuwa ni *mwanaumume*, mtu ambaye alikuwa thabiti na mtulivu.” Nami nikaendelea tu kuketi pale nikilia, na kuzungumza na Bwana, mikono yote miwili imeinuliwa, huku machozi yakitiririka mashavuni mwangu.

¹¹⁴ Nilisikia Sauti, ile Nuru kichakani, Naye akasema, “Nilikuumba kwa ajili ya, hivyo kwa kusudi fulani. Sasa, mnajua, kwamba hiyo... huwezi kuridhika mpaka bunduki hiyo, haidhuru mtu yeyote anasema nini, unajua inapiga shabaha, mnaona, kwenye yadi hamsini.” Ndipo Yeye akasema, “Hiyo ndiyo sababu nilikufanya hivyo, kwa sababu haileti tofauti yoyote yale mtu yeyote asemayo.” Mnaona?

¹¹⁵ “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu.”

¹¹⁶ Sikilizeni, upo, kwa sababu ninajua ndivyo ilivyo. Hao mitume walimchukua Roho Mtakatifu yuyo huyo, waliona

maono, wa—wakawafufua wafu, wakawaponya wagonjwa, wakafanya miujiza mikubwa, na ishara, na maajabu. Na kama tukililenga shabaha, huwezi kusema, “Loo, siku hiyo. . . Kanisa hilo linasema *hivi*. Nalo kanisa langu ndilo lililokuwa la kale kuliko yote, na *hili* lilikuwa *lile*,” hilo halina maana kwangu, ni kwamba kama walilifanya lilenge shabaha, litailenga tena.

¹¹⁷ Kama walikuwa wameleta uamsho wa kuutikisa ulimwengu kwa nguvu, na ahadi za Mungu, tutafanya jambo lile lile kama tutaikubali hiyo ahadi, na kutarajia itendeke. Lakini huna budi kuiamini, huwezi tu kuiamini nusu.

¹¹⁸ Nanyi mwajua nini? Nilipotoka chini ya mti huo baada ya Yeye kunena nami, na katoka hapo nje wala kamwe sikuigusa bunduki hiyo hata wakati mmoja, na huyu *hapa* ameketi mvulana ambaye tunatia risasi naye, bunduki hiyo daima imelenga shabaha kwenye yadi hamsini tangu wakati huo, hiyo ni kweli, kamwe sikuigusa. Mnaona, Yeye alikuwa akijaribu kunifanyia jambo fulani, kunionyesha jinsi ya kujimudu katika nyakati ngumu na mambo wanayosema, “Loo, Ndugu Branham. . .”

¹¹⁹ Jamaa fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, “Kama ungekuja huku na kujiunga na dhehebu letu, tutafanya *hivi na vile*, kama tu utapatana juu ya ninii chache. . .”

¹²⁰ Nikasema, “Ati kupatana? Kupatana?” Nikasema, “Ninashangaa sana kwamba mtu wa Mungu, kama ulivyo wewe, mwenye digrii ya udaktari, angemwomba mtumishi wa Mungu kupatana juu ya Neno la Mungu.” Nikasema, “Hilo halikai damuni mwangu.” La, bwana, nitadumu nimelilenga moja kwa moja.

¹²¹ Ninaamini katika Roho Mtakatifu na nguvu za Roho Mtakatifu. Ninaamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nami nina matarajio ya kwamba Yeye atainua Kanisa liende kumlaki likiwa na nguvu zile zile lilizokuwa nazo hapo mwanzo. Hakika, kama tutatarajia jambo hilo, tumwamini Mungu, na kuamini Yeye atafanya hivyo. Matarajio.

¹²² Musa, pamoja na theolojia yake yote, hakufika popote, alikuwa huko nje, mwoga, akikimbia nyuma ya milima, jangwani akiwachunga kondoo wa baba mkwe wake, lakini siku moja alikutana na Mungu, ndipo akapata tukio na Mungu, naye alikuwa akishuka kwenda Misri kuiteka Misri.

¹²³ Sasa, huenda likaonekana la kijinga sana kwa mzee, mwenye umri wa miaka themanini, huku masharubu yakinining’inia chini namna *hii*, na ninii yake, labda, kichwa chake chenye upara kimeng’ara chekundu kwenye jua, na ndevu zimejaa mwilini mwake, naye alikuwa na fimbo iliyopinda mkononi mwake, na mke wake ameketi juu ya nyumbu, na mtoto mdogo ameketi kwenye nyonga yake, akishuka chini.

Kasema, “Kwani unaenda wapi Musa?”

“Ninashuka kwenda Misri kuiteka, naenda kuliteka hilo taifa.”

¹²⁴ Unajua, unapoamini ahadi ya Mungu inakufanya utende kijinga kwa mambo ya ulimwengu. Sasa, uvamizi wa mtu mmoja, akishuka kwenda kuteka taifa kubwa kama Urusi ilivyo leo. Hakika, akishuka kwenda, na jambo, a—aliiteka, alifaulu.

¹²⁵ Alimwua mtu mmoja kule chini akaingia katika shida, akarudi huko chini, akaliua taifa zima na akatukuzwa kwake. Mnaona? Jambo ndilo hilo. Alikuwa mwuaji kwa kumwua mtu mmoja, kisha—kisha mtakatifu kwa kuua umati mzima. Lakini wakati mmoja alishuka akiwa na matarajio kujua ya kwamba Mungu alilitetea Neno Lake. Amina. Alikuwa akilitarajia.

“Utafanyaje jambo hilo, Musa?”

“Sijui, lakini mimi . . . Ninajua Yeye atafanya hivyo. Mungu alisema hivyo, hilo latosha, hamna lingine.”

“Ati utawaleta watu milioni mbili na nusu huku nje kwenye jangwa hili na kuwalisha? Utawalishaje?”

“Sijui, ninatarajia Mungu afanye jambo fulani kulihusu.” Alifanya, hivyo tu. Alikuwa akitarajia jambo fulani.

¹²⁶ Shida yake, tunaenda kanisani na kuimba wimbo, naye mchungaji anazungumza kuhusu waridi na maua, kisha tunarudi nyumbani. Loo, jamani! Hiyo ndiyo sababu hatufiki popote. Hiyo ndiyo shida ya makanisa yetu ya Kipentekoste. Hiyo ni . . . si—sikuja hapa kuwapigapiga mgongoni, nimekuja hapa, kuwaambia ukweli. Mnaona?

¹²⁷ Loo, kanisa la Kipentekoste limezama katika harakati za ujenzi, limezama katika vurugu za kimadhehebu, limeenda kila mahali, na kukatwa na kugawanyika, na kujiondoa, na kutengana, na kubaguana. Na loo, litakuwa na . . . “*Hili* litakuwa ndilo kubwa kuliko yote.” Na, “*Lile* litakuwa kubwa kuliko yote.” Maadamu mnafanya hivyo, kamwe, hamtafika popote, kumbukeni, ninawaambia katika Jina la Bwana.

¹²⁸ Lakini wakati mtakapokuja pamoja, loo, jamani, hivyo ndivyo, mtakapomtii Mungu kikamilifu, “Hivi watu wote watajua ya kuwa ninyi ni wanafunzi Wangu, mkipendana ninyi kwa ninyi.” Mtakapotoa sehemu ya theolojia nje na kuingiza upendo mdogo mle ndani, utafanya kazi, na maajabu, na—na miujiza, lakini hatuna budi kuwa na hiyo. Kwa nani? Kwa kila mtu.

¹²⁹ “Loo, kwa maskini kundi hilo la Assemblies of God, ama maskini kundi lile la Church of God, ama maskini wa Umoja, ama wa Utatu, ama Utano, ama chochote walicho nacho? Ati niwapende? Nisingeweza kuwapenda, wao ni mpinga-Kristo.” Wewe mwenyewe umepotea, ndugu, unapowazia hivyo, hiyo ni kweli, huko sawa na Mungu.

¹³⁰ Kama huwezi kuinua mkono wako kwa adui mbaya sana uliye naye, na kujaribu kumvuta kwa Kristo, basi Roho wa Kristo hayuko ndani yako. “Kwa kuwa alikuja kwa walio Wake, wala walio Wake hawakumpokea,” hata hivyo aliyatoa maisha Yake kwa ajili ya adui Yake, aliyatoa. Jinsi lilivyo kweli!

¹³¹ Na Roho huyo wa Mungu ndani yako hukufanya ujisikie vivyo hivyo kuhusu kila mtu. Unapofikia mahali . . . Sasa, huwezi tu kuliigiza, ibilisi anajua kama unaigiza au huigizi.

¹³² Ninaweza kumwona mtoto huyo mwenye kifafa huko nje siku moja, naye Yesu siku kumi kabla ya hapo aliwapa uwezo wa kutoa pepo, na—na kuwafufua wafu, na kuwaponya wagonjwa, na kufanya miujiza ya kila namna. Walikuwa wakiendelea vizuri sana, wakarudi, na kusema, “Hata pepo wanatutii,” wakiwa na wakati mzuri. Siku chache baadaye, hawa hapa wote walikuwa wameduwazwa.

¹³³ Walikutana na mtu huko chini, mwajua, ambaye hakuwa akifanya, asingekuja kujiunga na shirika lao, kwa hiyo wakamkataza hata kutoa pepo. Mnaona uchungu ukiingia? Mnaona? “Loo, tunamkataza, la, asingejiunga na kusanyiko letu, kwa hiyo tukamwambia, asifanye hivyo.”

¹³⁴ Yesu alisema, “Msifanye hivyo, hakuna mtu awezaye kufanya mwujiza katika Jina Langu, anayeweza kuninenea mabaya. Wala wao si kinyume Changu. . . walio upande Wangu, hawako kinyume Changu.”

¹³⁵ Kwa hiyo tunaona basi, juu ya mtazamo wa namna hiyo, walikuwa na mvulana mwenye kifafa kule chini, akimlilia tu, na kuomba, na kukanyaga-kanyaga, na—nami ninaweza kuwazia mmoja wao akija, na kusema, “Hivi ndivyo nilivyofanya hilo huko, ninyi ndugu rudini nyuma, nyote hamjui jinsi ya kufanya jambo hilo, hivi ndivyo mnavyolifanya.” Majivuno, mwajua, “Haleluya! Utukufu kwa Mungu!” Kamtikisa, kamtia mafuta kidogo, kamtikisa tena. “Hivyo ndivyo nilivyolifanya.” Uh-huh. Lakini halikufanya kazi wakati huo, hiyo ndiyo shida siku hizi, hiyo ndiyo . . . halifanyi kazi vizuri sana. Mnaona?

¹³⁶ Lakini baada ya kitambo kidogo, Mtu fulani akashuka akitembea, kimya kimya. Loo, baba alimkimbilia na kusema, “Bwana, mrehemu mtoto wangu. Yeye amepagawa sana na pepo.”

¹³⁷ Ndipo Yesu alipomtoa pepo mchafu, ndipo wanafunzi wakaja, na kusema, “Kwa nini tusingeweza kufanya hivyo? Kwani tulikuwa na shida gani?”

¹³⁸ Kamwe hakusema, “Nilizirudisha nguvu Zangu.” Alisema, “Ni kwa sababu ya kutokuamini kwenu kufanyiza kazi zile nguvu nilizowapa kuzifanyia kazi.” Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, limeachilia, linaninii . . . hali—halitarajii chochote, limeketi tu hapo, limenyong’onyea na limekufa. Tunachohitaji ni kuwa na matarajio.

139 Simeoni, maskini mtakatifu huyu mashuhuri wa Mungu, alikuwa ni mtu mwenye sifa kuu.

140 Loo, siku hizi hawana budi kusema, “Lakini ngoja kidogo, bwana, mimi ni mfanyabiashara. Mimi ni daktari. Mimi—mimi ni profesa.” Wewe si bora kuliko mtu mwingine yeyote. Na wakati wowote unapowazia wewe ni bora kuliko mtu mwingine, basi wewe si kitu unachopaswa kuwa, Maandiko yanasema. Unaona?

141 Unapofikia mahali...Huna budi...Mnawezaje kuwa na imani wakati mkitarajia heshima, mmoja kutoka kwa mwingine? Mnaona? Hamna budi kutangulizana, sikuzote, hayo ndiyo maisha ya Kristo, kumtanguliza ndugu yako, dada. Na kama wamekosea, hilo ni sawa, kamwe hamtawafanya bora zaidi kwa kuwapiga mateke huku na huku, mkumbatie, ukamnyanyue.

142 Ninapenda dini hii ya kale, nawaambia itakayofanya, ita—itamfanya aliyevaa suti ya gharama kubwa aketi karibu na aliyevaa ovaroli, na wakumbatiane, na kuitana *ndugu*, hiyo ni kweli; itamfanya aliyevaa kaliko na aliyevaa hariri waitane *dada*. Hakika itafanya hivyo. Imenyoka kama mtutu wa bunduki, na ni halisi, na bila shaka i—itamfanya hivyo.

143 Sasa, lakini Simeoni alikuwa mtu mwenye sifa kuu, alikuwa mzee mwenye hekima, yapata umri wa miaka themanini. Sasa, alikuwa akizunguka-zunguka akimwambia kila mtu, “Sitakufa mpaka nitakapomwona Kristo wa Bwana.” Sasa, Biblia ilisema...Ni kitu gani kilichomfanya Simeoni kufanya hivyo? Kwa sababu Roho Mtakatifu alikuwa juu yake, hiyo ndiyo tofauti, Roho Mtakatifu alikuwa juu yake.

144 Sasa, ninawazia lile dhehebu kuu alilokuwa mshiriki wake lilisema, “Loo, maskini jamaa huyo mzee, ana mguu mmoja kaburini, na huo mwingine unateleza upesi. Achaneni tu naye, haitachukua muda mrefu hata yote yatakakapokwisha. Atakufa hivi karibuni sana, kwa hiyo acha tu ajifurahishe, aendele mbele. Kidogo a—amedanganyika, kwa hiyo, kidogo ana kasoro, mwajua.”

145 Lakini Simeoni angali aliamini hilo, hakujali sifa zake, alimjulisha kila mtu. Alikuwa akitarajia kumwona. Akasema, “hataona mauti, mpaka nitakapomwona Kristo wa Bwana.”

146 Ninaweza kuwasikia baadhi ya marabi mashuhuri, mwajua, wakisimama, wale jamaa vijana, mwajua, waliojua ninii yote, waliokuwa na Ph.D. na ma-LL.D. na ma-D mengine yote, na kadhalika, nao wameshindiliwa zote, mwajua, na—nao wanasema, “Vema, maskini jamaa huyo mzee, amekuwa kuhani mzuri, mzee katika siku zake, lakini, loo, achaneni naye tu, kidogo amerukwa na akili.”

147 Lakini alikuwa akienda huku na huko akisimulia, hakujali sifa zake kama mtu mwenye hekima, kile alichokuwa akizungumzia, yeye—yeye alikuwa na Roho Mtakatifu juu yake, akasema, “Roho Mtakatifu alinifunulia.” Mnaona,

alikuwa akitarajia kuiona. Kasema, “Naam, nimeandaa kila kitu, nitakapomwona Yeye, ninajua tu kile nitakachofanya. Naam, bwana. Nimeandaa kila kitu, kwa sababu ninatarajia kumwona.” Kwa nini? Roho Mtakatifu alisema hivyo.

¹⁴⁸ Sasa, hakuna Roho Mtakatifu wawili, kuna Roho Mtakatifu mmoja tu, hiyo ni kweli, Roho Mtakatifu mmoja tu. Naye Roho Mtakatifu yule yule aliyemwongoza Simeoni kuamini ya kwamba hatakufa mpaka amwone Kristo wa Bwana, Roho Mtakatifu yuyo huyo ananiambia, “Jambo fulani litatukia.” Amina. Ninaliamini tu.

¹⁴⁹ Naye anakwambia jambo lile lile. Hebu tuwe tukilitarajia, hebu tujiweke tayari kwa ajili yake, tujitayarishe. Kama vile kufanya safari, kupakia kila kitu, la, safari ya namna hii—hii, unapakua kila kitu, tumepakia vitu vingi kupita kiasi sasa, ndiyo shida yake, hatuna budi kuvipakua. Kwa hiyo, safari hii unapakua. Inakubidi kuingia moja kwa moja katikati ya barabara.

¹⁵⁰ Mmoja wa hao ndugu wapendwa, Ndugu, nilikuwa nikitaka kusema DeWeese, ninaamini, la, la, huyo ni Oral Roberts. Loo, yeye ni msimamizi wa jimbo la Assemblies of God huko Indiana, ninasahau jina lake sasa. Kwa vyovyote vile, Ndugu Weed, Roy Weed, nadhani nyote mnamfahamu. Ndugu Weed, siku moja . . .

¹⁵¹ Binamu yangu, Ndugu Vibbert, ana moja ya makanisa makubwa sana ya Pentecostal Assembly of God mashariki huko Evansville, Indiana, ana bloku nzima za mji zilizofanywa tu kanisa, mkutano. Kwa hiyo, walikuwa na, ninaamini kiliitwa Chumba cha Mia Tano. Ng’ambo ya barabara kuna gereji, kwa hiyo Ndugu Vibbert ndiyo kwanza ainunue, naye ndugu yake, wakishindana huko Indianapolis, ni nani anayeweza kuwa na elfu *ngapi* katika shule ya Jumapili. Kwa hiyo, alikuwa na shule ya wanaume kule ambayo aliifundisha tu Jumapili asubuhi, mia tano darasani.

¹⁵² Kwa hiyo nilipaswa kuzungumza asubuhi hiyo kwenye darasa la wanaume. Nilikuwa nimeketi nyuma ya Ndugu Roy, ndipo Ndugu Roy akasema, “Unajua, nilimsikia mtu akisema,” na huyo alikuwa ni mimi, “kwamba ninii—katikati ya barabara ndipo mahali, kasema, ‘Katikati ya barabara . . .’” Ninaamini hilo.

¹⁵³ Mungu alisema katika Isaya 35, “Kutakuwako na njia kuu.” Wengi wenu ninyi Wanazarayo wapendwa mlikuwa mkiimba, “Njia kuu ya utakatifu.” La, “Kutakuwa na njia kuu na” *na* ni kiunganishi, kinaunganisha sentensi yako pamoja, “na njia, nayo itaitwa, *Njia ya utakatifu*,” si *njia kuu ya utakatifu*, *njia*. Barabara sahihi imejengwa ili kwamba ifagilie mbali takataka upande mmoja au mwingine. Kwa hiyo, ama utakuwa baridi sana na mgumu, ama mlokole kwenye . . . Lakini njia iko moja kwa

moja katikati ya barabara, moja kwa moja kuelekea Kalvari, moja kwa moja barabarani.

¹⁵⁴ Kwa hiyo Ndugu Weed akasimama, na kusema, “Mtu, hayo siyo maadili mema ya kuendesha gari,” akasema, “kama mtu akiendesha gari katikati ya barabara, angeuawa.” Kasema, “Hayo si maadili mema ya kuendesha gari.”

¹⁵⁵ Hakujua nilikuwa nimeketi nyuma yake. Nikamgusa begani, nikasema, “Jambo ndilo hilo, Ndugu, wewe ni mtu wa duniani sana, wewe ni...” Nikasema, “Barabara hii, huirudi, ni barabara ya kwenda upande mmoja tu inayoelekea *kule*.”

¹⁵⁶ Na kwa hiyo, yeye ni—yeye ni ndugu mzuri, mzuri tu kama ilivyoweza kuwaziwa. Loo, jamani, hawa—hawawafanyi vizuri kuliko Roy Weed. Lakini lilipendeza sana, mwajua, alisema, “Sasa, ukiendesha gari katikati ya barabara utagongwa.”

¹⁵⁷ Nikasema, “Ndugu Weed, hatutagongwa, tunaenda njia moja, nyoofo, moja kwa moja tu, hatutarudi nyuma hata kidogo.” Tiketi ya kwenda tu, nina furaha ninayo basi, na wewe je? Tikiti ya kwenda bila kurudi.

¹⁵⁸ Kile Roho Mtakatifu anachofunua kupitia Neno Lake, ninaamini hicho ni kweli, nasi tunadumu moja kwa moja nacho. Kwa hiyo, Simeoni alikuwa mtu mwenye sifa kubwa miongoni mwa watu, bali hakuona haya. Baadhi yetu tunadai kuwa na Roho Mtakatifu, tunapata ufunuo kutoka kwa Mungu kwamba tunapaswa kuacha kufanya mambo tunayofanya, “Lakini hata hivyo nikimpata, ni—nikitembea kote na akina Jones huku, wataniwazia nini?”

¹⁵⁹ Baadhi yenu wanawake mlikata nywele zenu, mwajua, kwa sababu Susie alifanya hivyo, “Vema, kama nikiachilia nywele zangu zikue, wageniita wa mtindo wa kale.” Um-hum. Lakini Roho Mtakatifu anakwambia unapaswa kufanya hivyo, Biblia ilisema hivyo. Sasa, kama jambo lolote likisema kinyume na hilo, usiliamini, ni uongo, kwa sababu Mungu alisema ilikuwa hivyo. Unaona? Na upuuzi huu mwingine wote ambao tumeingiza katika kanisa la Kipentekoste kwa sababu Wabaptisti walifanya hivyo, kwa sababu Presbiteri hufanya hivyo, “Nao watafikiri mimi ni mlokole wa mtindo wa kale.”

¹⁶⁰ Kuona wanawake wetu wa Kipentekoste wamevaa nguo zinazoonekana kana kwamba zinabana sana, mwanamke fulani aliniambia hivi majuzi, kasema, “Lakini Ndugu Branham,” akasema, “vema, hawashoni chochote tofauti na hizo.” Lakini wana cherehani na vitambaa, kwa hiyo hakuna udhuru.

¹⁶¹ Yesu alisema, “Kama wewe...” Hmm! Yesu alisema, “Ukifanya hivyo, utakuwa na hatia kwenye Siku ya Hukumu kwa kufanya uzinzi.” Biblia ilisema, “Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye tayari moyoni mwake.”

¹⁶² Nawe ukivaa hivyo, naye mwenye dhambi akuangalie, yeye atawajibika kwenye Siku ya Hukumu, nawe utawajibika kwa kujianika hivyo kwake, kwa hiyo utakuwa na hatia ya kufanya uzinzi, kama ulifanya tendo hilo au la, kwa sababu, kasema, “Kila amtazamaye,” nawe unajionyesha mwenyewe, mwenye dhambi kweli atafanya hivyo. Loo, enyi kanisa la Kipentekoste, mrudieni Mungu! Rudini.

¹⁶³ Loo, ilikuwaje tangu Mtaa wa Azusa hadi wakati huu? Mtaa wa Azusa, ilikuwa ni aibu kuwa na kitabu cha nyimbo ka—kanisani wakati Pentekoste ilipoanza. Waliimba katika Roho, kila kitu kilikuwa katika Roho. Sasa ni kama vile David duPlessis alivyosema, “Tuna wajukuu wengi kupita kiasi wa Kipentekoste.” Mungu hana wajukuu wowote hata kidogo, Yeye anao tu wana na mabinti.

¹⁶⁴ Uliwaleta watoto wako kanisani, kwa sababu tu wewe ulikuwa Mpentekoste, watoto wakaingia, na kupata malezi, wakakua na kudai Pentekoste, wala hawajui lolote kuhusu tukio lililowafanya wanawake wajisafishe, na wanaume kujisafisha, na makanisa kujisafisha. Afadhali nifunge domo, pia, ama... Lakini ni kweli. Hatuna budi kurudi kwenye tukio hilo tena. Vema. Ninamtarajia kufanya jambo fulani kabla hajaja, nami na—naamini nitaliona. Vema.

¹⁶⁵ Lakini ilifunuliwa kwake, hiyo ndiyo sababu angeweza kusimama juu ya Neno, akasema, “Roho Mtakatifu alinifunulia ya kwamba sitakufa, ninajua mimi ni mzee, lakini sitakufa kabla sijamwona Kristo wa Bwana.” Ambaye Daudi alimtamazia, naye Musa akamtazamia, na tangu bustani ya Edeni, miaka elfu nne, walimtamazia, bali yeye alisema, “Nitamwona.” Amina. “Nitamwona.”

“Unajuaje utamwona?”

“Nina sababu nzuri: Roho Mtakatifu alinifunulia.” Loo, jamani!

¹⁶⁶ Je, Yeye anakufunulia huko nje kwenye machela usiku wa leo, ndugu, Yeye (ama huko nje kwenye hivyo viti) atakuponya? Kama akikufunulia, utaupata, hivyo tu. Je, Yeye anakufunulia, ewe mwenye dhambi, ya kwamba utampokea Roho Mtakatifu? Utampata kama Yeye akilifunua. Wewe uliye na ugonjwa wa moyo, kansa, uvimbe, chochote kile, umefunuliwa kwamba utaponywa? Utaupata, fuata tu huo mwongozo.

¹⁶⁷ “Wana wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu,” si kuongozwa na walokole wengine, ama madhehebu fulani, ama *kitu fulani*, wanaongozwa na Roho wa Mungu. Roho Mtakatifu alipewa Kanisa apate kuwa Mwangalizi, yule Mwalimu ambaye alipaswa kuwalea watoto wa Mungu, si maaskofu wetu, na makadinali, na kadhalika, bali Roho Mtakatifu.

¹⁶⁸ Ninamtarajia Roho Mtakatifu, si dhehebu, si askofu, si kasisi wa Katoliki, si mhubiri wa Kibaptisti, ama mhubiri wa

Kipentekoste, ninamtarajia Roho Mtakatifu kushuka na kuweka katika utaratibu Kanisa litakaloenda kumlaki, lililojazwa na nguvu na ufufuo wa Kristo. Ninatarajia hilo, ninaliamini. Mungu aliliahidi hilo, ya kwamba kungekuwako na Kanisa pale lisilo na waa wala kunyanzi juu Yake. Ninalitarajia, kwa sababu Mungu alisema ndivyo ilivyo.

¹⁶⁹ Mtu fulani aliniambia, “Ndugu Branham, hivi huogopi unaweza kufanya kosa usiku fulani huko juu, kwenye huo upambanuzi?”

La, bwana. Yeye aliniambia atasimama pamoja nami, ninamtarajia kufanya hivyo. Hiyo ni kweli kabisa.

“Hivi huogopi baadhi ya hizo nabii zitakuwa ni za uongo?”

¹⁷⁰ Kama ningeogopa, ningeacha kulisema kama halikuwa, nilikuwa na imani katika Yule aliyekuwa akizungumza nami, bali ninatarajia iwe hivyo. Yeye alisema atafanya hilo, nami ninaninii, halijashindwa bado, wala halitashindwa kamwe, kwa sababu ninamtarajia atimize Neno Lake, lililofunuliwa na Roho Mtakatifu. “Wana wa Mungu, wanaoongozwa na Roho wa Mungu.”

Sasa, hebu na tuchukue mchezo mdogo wa kuigiza kabla hatujafunga.

¹⁷¹ Je, mtakuwa mkitarajia ibada kuu ya uponyaji kesho usiku? Je, mtakuwa mkimtarajia Bwana kumwaga baraka Zake kesho usiku? Hakika, hebu tuwe tukilitarajia, tuwe chini ya matarajio. Loo, natarajia kanisa liwake moto, utukufu wa Bwana ukishuka kila mahali, na wenye dhambi kuzunguka madhabahu, na watu wakiokolewa, na kujazwa na Roho Mtakatifu, na ni jambo kuu tu.

¹⁷² Matumaini yangu na matarajio yangu yamepanda juu sana. Nilijisikia kuongozwa kuja, California, na Yeye atamfanyia mtu fulani jambo fulani, hilo ni jambo moja la hakika. Ninatarajia jambo hilo litukie, kwa sababu ninajisikia kuongozwa kufanya hivyo. Ninajisikia kuongozwa kusema yale ninayosema, ninajisikia kuongozwa kufanya mambo ninayofanya, la sivyo nisingeyafanya. Ninataka kuongozwa Naye, halafu ninatarajia jambo fulani litukie.

¹⁷³ Sasa, hebu tuseme ni Jumatatu asubuhi, kuna yapata watu milioni mbili na nusu katika Israeli wakati huu, wako chini ya serikali ya Kirumi. Ndipo mzee Simeoni anaingia, jukumu lake lilikuwa, labda, kufanya jambo fulani kanisani, na baada ya kitambo kidogo huyu hapa amesimama kule nyuma, naye anachukua Gombo, naye ameketi kwenye chumba chake cha kusomea, huyo mzee bado hajatoka.

¹⁷⁴ Yeye ni mzee, mzee sana, naye alikuwa amesimama pale, akachukua Gombo, na asubuhi hiyo, hebu tuseme alifungua Isaya, akasoma akafikia yapata Isaya 9:6, “Kwa maana kwa ajili

yetu Mtoto amezaliwa,” (Loo!) “tumepewa mtoto Mwanamume, ataitwa Jina Lake Mshauri, Mungu Mwenye Nguvu, Mfalme wa Amani, Baba wa Milele.”

¹⁷⁵ “Loo, nabii alikuwa akinena habari za Nani? Huyu ni yule Masihi atakayekuja, huyo Ndiye ambaye Roho Mtakatifu alinifunulia ningemwona.”

¹⁷⁶ Sasa, hawakuwa na televisheni, Mungu ashukuriwe, katika siku hiyo, kwa hiyo, propaganda za namna zote, habari, na magazeti, na ripoti, hawakuwa nazo. Yesu alikuwa tayari amezaliwa. Kwa hiyo, siku nane baadaye... nadhani katika watu milioni mbili na nusu, kungekuwako na mamia ya akina mama huko asubuhi, kwa ajili ya watoto wao wa kiume kutahiriwa.

¹⁷⁷ Vema, jinsi ambavyo mama peke yao, mnajua jinsi wanavyowapenda watoto wao, wanawapapasa kidevuni mwao, wasio na meno. Ninapenda tu kumwona mtoto mchanga asiye na meno, mwajua, maskini fizi ndogo tu ziking'ara. Nami ninaweza kuwazia akina mama wakisimama pamoja na watoto wao wachanga, wakiwa na mablanketi mazuri ya ushonaji, na *kuwapapasa* mashavuni namna *hiyo*.

¹⁷⁸ Ndipo maskini bikira akaja akitembea huku Mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto. Nami naambiwa, kulingana na historia, kwamba nguo za kitoto za Bwana wetu zilitolewa nyuma ya nira ya maksai, zilizokuwa zimening'inizwa zizini. Walikuwa wakilima kwa nira hii, kwa hii, nao wakaifungua hii, na kumfunika huyo Mtoto mchanga kwayo.

¹⁷⁹ Nami ninaweza kuwazia nikiwaona hao wasichana wa jamii, baadhi ya walio bora sana wa Hollywood, wakitembea pale, mwajua, wamesimama kanisani, majina kwenye kitabu, loo, jamani, wao ni wafuasi maarufu, huku watoto wao wachanga wametiwa manukato kabisa, na, mwajua, na mishono, na vijibuti vidogo, na kila kitu tayari, mwajua, wakitembea tu.

¹⁸⁰ Na jinsi ambavyo kuhani atajua walikuwa ni watoaji hodari kwenye sahani na, mwajua, “Naam, Bibi *Nanii*, mume wako ni Daktari *Nanii*,” namna hiyo, mwajua. Jinsi wangepokea heshima hiyo, loo, jamani, wote wanajivunia hilo.

¹⁸¹ Ndipo maskini msichana huyu anaingia pamoja na Mtoto mchanga aliyefungwa kwa kitambaa kilichotolewa nyuma ya nira ya maksai.

¹⁸² Nami ninawasikia baadhi yao wakisema, “*Shh!* Umesikia huo umbeya, sivyo? Hujasikia huo umbeya? Msichana huyo alipata mtoto huyo kwa Yusufu, bila kuolewa naye. *Hmm!* Loo, ni mbaya sana, loo, ni... Wewe—wewe... Ni vibaya sana! Unaona? Loo, ni—ni—ni—ni fedheha! Naye anasema amezaliwa na bikira.”

183 Hakujali, alishika maskini Hazina yake ndogo mkononi mwake, alijua moyoni mwake kwamba Mtoto huyo alikuwa ni wa Nani, alijua Huyu alikuwa ni Mwana wa Mungu. Haidhuru ni wangapi waliocheka, na kusema, “Usi—usimkaribie, watu wakikuona ukishirikiana naye, basi watakuhesabu kama mmoja wao.”

184 Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Ninahofia hilo ndilo linayapata makanisa yetu ya Kipentekoste, hutaki kuwa mmoja wao, tena, hutaki tukio hilo la mtindo wa kale la ubatizo wa Roho Mtakatifu, na Moto na nguvu za Mungu. Tuseme... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... mtindo wa kale, pia. Hiyo ni kweli kabisa.

185 Sasa, akatembea pale, moyoni mwake alijua Mtoto huyo alikuwa ni wa Nani, acha waseme watakalo, yeye alijua huyo Mtoto alikuwa ni wa Nani. Na vivyo hivyo unajua mahali ujuzi huo unakotoka, huyo Mtoto mchanga, Kristo, aliyezaliwa moyoni mwako, huionei haya Injili ya Yesu Kristo.

186 Paulo alisema, “Siionei haya Injili ya Yesu Kristo, kwa kuwa ni nguvu za Mungu ziletazo wokovu.” Ninapenda hilo, naam, bwana.

187 Wakati alipokuwa amesimama akizungumza na Festo siku hiyo, ama Feliki, naamini ndiye, alisema—alisema, “Wewe karibu unishawishi kuwa Mkristo.”

188 Naye Paulo alikuwa amemwambia, kasema, “Kwa njia inayoitwa uzushi,” huo ni *wendawazimu*, *kichaa*, “hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa Baba zetu.” Nina furaha kuungana naye usiku wa leo, nanyi je, enyi Wapentekoste? Hivi hamna furaha, usiku wa leo, kusema, “Mimi ni mmoja wao?”

Palikuwa na wimbo mdogo wa Kipentekoste tungeuimba:

Walikuwa wamekusanyika katika chumba cha
juu,
Wote wakiomba katika Jina Lake,
Wamebatizwa kwa Roho Mtakatifu,
Ndipo nguvu za huduma zikaja;
Yale aliyowafanyia siku hiyo
Atakufanyia vivyo hivyo,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Hivi hamna furaha kwa hilo? Loo, nina furaha sana kwamba mimi ni mmoja wao.

189 Akatembea pamoja na Mtoto huyo mchanga, huku wote wakisema, “Usimkaribie sasa. Ah, yeye ni mtakatifu anayejibingirisha,” ama—ama mwajua, kitu kama hicho. Angalia tu... Labda nilisema jambo baya wakati huo, bali natumaini sikusema.

¹⁹⁰ Kwa hiyo, alijua Mtoto huyo mchanga, alijua ni wa Nani, alijua Huyu alikuwa ni Mwana wa Mungu, haidhuru ni fedheha jinsi gani. Nawe unajua ya kwamba kama umewahi kumpokea Roho Mtakatifu, unajua ya kwamba hilo ni tukio la Mungu kwako, unajua unakotoka, unajua shimo ulimotolewa, unajua kilichokuokoa, unajua kilichokufanya tofauti.

¹⁹¹ Naye akaendelea, “Hiyo ni sawa wanayosema, sitasikiliza hata kidogo, nitakuangalia tu Wewe, Kipenzi.”

¹⁹² Loo, laiti kanisa la Kipentekoste lingeweza tu kumpenda Kristo namna hiyo, “Bwana, nitakuangalia Wewe, Mpenzi. Wewe ni Kipenzi cha Mungu. Nimekatajiwa. Nitajifanya. . . Nitafanya mwenendo wangu kama Mkristo halisi, nitatembea katika Nuru ya msalaba, huku nimenyosha mkono wa upendo na utamu.”

¹⁹³ “Naam, najua Wewe ni wa Nani, Kipenzi, Wewe ni Zawadi niliyopewa na Mungu.”

¹⁹⁴ Basi muda si muda mwajua, maskini mzee Simeoni ameketi chumbani, Isaya 9:6, naye Roho Mtakatifu. . .

¹⁹⁵ Sasa, angalia, kama Roho Mtakatifu amekuahidi jambo fulani, nawe umekuwa ukilitarajia, ni juu ya Roho Mtakatifu basi, kuhakikisha kwamba unaongozwa kwake. Ni wangapi wamekuwa wakitarajia uamsho? Vema. Sasa, labda huu ndio wakati Yeye amekuongoza kwake. Kama kuna uamsho unaoandaliwa, Yeye atakuingiza moja kwa moja ndani. Ni wangapi wamekuwa wakitarajia uponyaji? Hakika, vema, basi wewe huyu hapa moja kwa moja kwenye chemchemi.

¹⁹⁶ Angalieni, ninii. . . Daudi alisema, “Kilindi kinapoita kilindi.” Kama kuna kilindi ndani kinachoita, hapana budi pawe na kilindi mahali fulani cha kuitikia kilindi hicho. Mnaona ninalomaanisha? Kabla ya kuwapo, hapa, ninyi ni watu, mnaishi kando ya bahari, kabla hapajakuwapo na pezi mgongoni mwa samaki, ilibidi kuwe na maji kwanza apate kuogelea, la sivyo kamwe asingekuwa na pezi. Kabla hapajakuwapo na mti wa kukua ardhini, ilibidi kuwe na ardhi kwanza, la sivyo kusingekuwa na mti wa kukulia humo.

¹⁹⁷ Kama vile nimetoa tamshi hili mara nyingi, nilisoma makala, gazeti hilo wakati fulani uliopita, kwamba mvulana mdogo shuleni aliendelea kula vifutio kutoka kwenye penseli yake, nao wakatuma mtu nyumbani, na kumwuliza mama yake maskini jamaa huyu mdogo ana shida gani. Ndipo siku moja akamkuta huko nje akila pedali ya baiskeli.

¹⁹⁸ Kwa hiyo, alimpeleka kwenye maabara kuninii, ama kliniki, hasa, kufanyiwa uchunguzi wa damu ya—yake, na kadhalika. Kwa hiyo, walipomchunguza maskini jamaa huyo, walikuta kwamba alihitaji salfa, maskini mwili wake ulikuwa ukitamani salfa, kwa hiyo salfa iko kwenye mpira. Kwa hiyo, sasa angalia, kabla hapajakuwapo na shauku ya salfa, ilibidi kuwe na salfa, kwanza, kuitikia shauku hiyo. Kwa maneno mengine, kabla ya

kuwepo na uumbaji, hapana budi kuwe na Muumba wa kuumba huo uumbaji. Mnaona ninalomaanisha?

¹⁹⁹ Sasa, kama unaona kiu zaidi kwa ajili ya Mungu... Ni wangapi wangetaka kuwa na Mungu zaidi? Vema, inakuonyesha kuna wingi zaidi wa Mungu kwa ajili yako. Hiyo ni kweli. Unataka kuponywa? Mbona, kwa hakika tu kama unavyoamini ya kwamba Mungu ni Mponyaji, kuna Chemchemi iliyofunguliwa mahali fulani, la sivyo kamwe hungekuwa na shauku hiyo. Kama unatamani kuwa na Roho Mtakatifu, hiyo inaonyesha kuna Chemchemi iliyofunguliwa mahali fulani, iliyojazwa na Roho Mtakatifu. Mnaona, inabidi kuwe na Muumba wa kuumba viumbe, halafu inabidi kuwe na kitu fulani huko nje kuitikia uumbaji huo.

²⁰⁰ Sasa, Roho Mtakatifu aliwajibika wakati huo, kumwongoza kwenye Chemchemi hiyo. Amina. Loo, kama unamtarajia, Roho Mtakatifu yuyo huyo hukuongoza kwenye Chemchemi hiyo, haina budi kufunguliwa mahali fulani. Kama una shauku hiyo inayowaka moyoni mwako, Roho Mtakatifu anawajibika kukuongoza Kwake, moja kwa moja kwenye Chemchemi hiyo iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambapo wenye dhambi, ambao ni wasioamini, wakitumbukia chini ya gharika hiyo, wanapoteza kutokuamini kwao kwote. Hiyo ni kweli.

²⁰¹ Loo, unataka kufikia mahali ambapo unaweza kupita shaka lolote niani mwako. Hivi hutaki kuwa hivyo? Vema, kuna Chemchemi, mahali fulani, kufanya hivyo. Unaitafuta, unaitafuta.

²⁰² Sasa, basi wakati huo, kama umekuwa ukiitafuta, ukishuhudia habari zake, ukiitarajia kwa sababu ilikuwa ni ahadi, na kila ahadi katika kile Kitabu ni yako, kwa hiyo umekuwa ukiitafuta, basi kama ilikuwa karibu naye, ilikuwa ni wajibu wa Roho Mtakatifu kumwongoza mahali hapo ambapo Kristo alikuwa. Hilo ni jukumu la Roho Mtakatifu.

²⁰³ Sasa, kama unaamini katika uponyaji, ni wajibu wa Roho Mtakatifu kukuongoza moja kwa moja hadi kwenye hiyo Chemchemi. Sasa, si lazima uingie, bali Yeye ataliongoza, akuonyeshe. Kama unamtafuta Roho Mtakatifu, ndipo Roho Mtakatifu atakuongoza moja kwa moja hadi mahali ambapo unaweza kumpokea Roho Mtakatifu, ukimruhusu tu akuongoze.

²⁰⁴ Ninaweza kumsikia Roho Mtakatifu chumbani asubuhi hiyo kwa Simeoni, akisema, "Simama!"

"Unataka niende wapi, Bwana?"

"Si kazi yako kujua, endelea tu kutembea."

Huyu hapa anakuja, hajui anakoenda, anatembea tu. Anatoka anaingia chumbani, anaangalia pande zote.

"Endelea tu kutembea, Simeoni."

“Wapi, Bwana?”

“Endelea tu kutembea.” Nitasema! “Endelea tu kutembea.”

“Nifanye nini?”

“Endelea tu kutembea, nitakuongoza.”

205 Je, uko tayari kumwacha afanye hivyo? Si kuchukua nia yako mwenyewe, chukua tu nia Yake. “Nia iliyokuwamo ndani ya Kristo na iwe ndani yenu.” Usikosoe, kama huwezi kulielewa, lichunguze katika Maandiko uone kama ni kweli ama si kweli. Unaona?

“Endelea tu kutembea.”

206 Anaenda kwenye mlolongo huu wa wanawake, labda kulikuwa na mia tatu ama mia nne wao wamesimama pale, ninamwona akitembea kwenye mlolongo, “Bwana, ni la kigeni, Wewe uliniambia siku moja, na Wewe, Roho Mtakatifu juu yangu, ulinifanya kujua mambo mengi. Hujawahi kunipungukia, sijui unataka nini kwangu asubuhi ya leo, lakini Wewe uliniambia niendele tu kutembea, kwa hiyo mimi huyu hapa.”

207 Akitembea, baada ya kitambo kidogo, mara macho yake yalipomwangukia maskini mwanamke huyo, wote wakisimama nyuma, kama vile waaminio wakwamia mpakani, mwajua, wakisimama nyuma kando, “Siku za miujiza zimepita,” na kadhalika, lakini mnajua, kwa moyo wenye njaa ambao unaongozwa na Mungu, wanajua mahali ulipo wanapoupata, wa—wanajua wamefika mahali fulani.

208 Kwa hiyo Simeoni, alipofika kule karibu na mahali alipokuwa Mtoto huyu mchanga, ninaweza tu kumwona yule mzee mwenye hekima, na machozi makubwa, yanayometameta yakidondoka kutoka kwenye mashavu yake yenye ndevu, kisha akanyosha mikono, na kumshika huyo Mtoto mchanga mikononi mwake, akaangalia juu Mbinguni (Loo, ni hisia ya jinsi gani!), “Bwana, sasa mruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani, kulingana na Neno Lako, kwa kuwa macho yangu yameuona Wokovu Wako.” Kitu kile kile ambacho kila mtu alikuwa akikikosoa, akikifanyia mzaha, huo ni Wokovu Wako. “Jalia mtumishi Wako sasa aondoke kwa amani, kulingana na Neno Lako, niko tayari kwenda sasa, kwa kuwa macho yangu yameuona Wokovu Wako.”

209 Huko nyuma kabisa pembeni kulikuwako na nabii mke mzee, kipofu, bali angeweza kuona moja kwa moja kupitia kwenye kuta hizo, kwa sababu alikuwa ni nabii mke, yeye pia alikuwa akingojea faraja ya Israeli. Naye Roho alikuwa juu yake, kipofu, amelala pembeni, akasimama, hapana shaka Roho Mtakatifu alisema, “Simama, Ana.”

210 Huyu hapa anakuja kupitia hekaluni, kipofu kimwili, lakini angeweza kuona mbali sana kuliko wengi wao waliokuwa wamesimama pale wenye macho mazuri. Loo, huo ndio uweza

wa kuona ninaotaka! Huyu hapa anakuja, akizungukazunguka jengoni, kipofu, naye akaja moja kwa moja, kuelekea mahali Mtoto huyo mchanga alipokuwa. Loo, jamani!

²¹¹ Akainua mikono yake na kumbariki Mungu, akambariki Mariamu, akatabiri, papo hapo mbele zao, kwamba huyo Mtoto atakuwa wa kuanguka na kuinuka tena na wengi katika Israeli, na yote, jinsi upanga pia ungeuchoma huo moyo, na jinsi manabii walivyokuwa wamesema jambo hilo lingetukia.

²¹² Sasa, kama maskini mwanamke huyo kipofu angeweza kuongozwa hadi mahali hapo bila macho ya kawaida, kuona Chemchemi hiyo iliyojaa Damu, ni zaidi sana vipi anavyoweza kuungoza kwenye msalaba, usiku wa leo, wewe uliye na macho mazuri, kuona kwa jicho lako la kiroho?

²¹³ Usitafute kushangiliwa na ulimwengu, hutakupata, bali uwe tayari kupoteza sifa zako. Kila kitu ulicho, kisalimishe kwa Ufalme wa Mungu. Utoe wakati wako kwa ajili ya maombi, ujitoe mhanga maisha yako, uachane na mchezo wako wa karata, uachane na mambo yote ya ulimwengu, umpe ibilisi, umwache ayachukue, ni mali yake, wewe tembea pamoja na Kristo.

²¹⁴ Wakati mmoja, miaka michache iliyopita, kulikuwa na mwanamuziki mashuhuri wa Kimarekani aliyezuru Urusi, naye akacheza lele huko Moscow. Nao walisema kwamba aliicheza kwa ustadi mkubwa, huku akiwa mwenye kipaji mashuhuri jinsi alivyokuwa, mpaka kusanyiko likasimama kwa maelfu na kupiga mayowe, na kuchapa miguu yao, na kupiga mayowe wakitaka acheze tena. Naye huyo mvulana akasimama tu pale, naye akaendelea tu kuangalia namna *hiyo*. Vema, wao, wote wakaanza kushangaa alikuwa na shida gani. Kwani hangepokea shangwe zao? Wote walikuwa wakishangilia.

²¹⁵ Hiyo ndiyo shida siku hizi, tunamtafuta mtu wa kujaribu kutupigapiga mgongoni, akisema, “Loo, wewe ni *hiki*, *kile*.” Usimtafute huyo, ulimwengu kamwe hautafanya hivyo. Kama papaso likija litakuwa moyoni na Bwana Yesu, mnaona. Usitazamie ulimwengu useme, “Loo, Bibi Jones, yeye ni mzuri. . .” La, la, usitafute hilo, utakosolewa.

²¹⁶ “Wote wanaoishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa,” kumbukeni tu. Kama hayaji, kuna kasoro, mahali fulani, chunguza, rudi, uone mahali tulipoachia.

²¹⁷ Tunatazamia kitu fulani cha kusema, “Tuna. . . sisi ni wafuasi wa shirika lililo kubwa kuliko yote katika Pentekoste. Sisi ni wafuasi wa *hili*, ama sisi ni wafuasi wa *lile*.” Mnaona? Usitazamie hilo, ukifanya hivyo, unaiacha ile barabara nyembamba, iliyonyoka.

²¹⁸ Mtu huyu, walikuwa, walikuwa wakishangilia, na kupiga mayowe, na kusema, “Anapaswa kuinama, hiyo ni kweli, ‘Loo, asanteni nyote, sana. Asanteni nyote, sana. Nitacheza moja bora zaidi wakati huu.’” Lakini hakuwa akifanya hivyo.

219 Nao wakanyamaza, wote wakaangaliana, nao wote wakapiga makofi tena, na kuchapa miguu yao. Lakini mvulana huyo kamwe hakujali kuchapa kwao miguu yao, au kupiga makofi yao. Ilitokea kwamba waliona, alikuwa ameyaelekeza macho yake juu namna *hiyo*, huko juu sana kwenye roshani. Nao wakaangalia juu kule kuona, maskini mwalimu wake alikuwa ameketi pale juu, yule mzee bingwa wa muziki. Alitaka kujua kile *yeye* atakachosema juu yake, hakujali yale waliyosema, alitaka kujua yale *yeye* aliyosema juu yake.

220 Nami nafikiri hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwazia katika uamsho huu ujao, hebu tusiwazie yale ulimwengu utakayowazia, hebu tuendeele kuangalia juu, tuone kile Bwana atakachosema, Bwana aliyetupa Roho Mtakatifu, Bwana aliyetufundisha kuishi maisha mema, Bwana aliyetupa Neno Lake, Bwana aliyetupa Maisha Yake. Na tumwishie Yeye aliyekufa kwa ajili yetu, wala tusiusikilize ulimwengu, bali tuone kile Yeye anachosema juu yake.

221 Juu ya hilo, hebu na tuje kesho usiku tukiwa na matarajio makubwa kuona dhihirisho la Mungu akiwaponya wagonjwa na wanaoteseka. Na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu.

222 Je, mko chini ya matarajio, enyi kanisa? Je, mnamtarajia Mungu kumwaga Roho Wake? Kuna mwenye dhambi hapa angetaka kuanza, usiku wa leo, kuja madhabahuni, na kusema, “Ninataka kupiga magoti, kuomba, Ndugu Branham, ni—ninamtarajia Mungu aniokoe usiku wa leo, ni—ninaingia kwenye mlango huo nikiwa na matarajio hayo?” Kama uko hapa, njoo.

223 Ni kitu gani kilichokuongoza mlangoni, mwanangu? Ni kitu gani kilichokuongoza mlangoni, ewe msichana? Ni kitu gani kilichofanya hivyo? Ni kitu gani kilichokuondoa kwenye umati huo wa matineja wa watu wasiojali ulimwenguni?

224 Nilipoingia mjini hivi majuzi usiku, kama tu, karibu, genge la majambazi limesimama hapa nje mahali fulani, wamevaa jaketi za pikipiki, suruali zilizoshushwa nusu nyongani mwao, na wengine, nywele za kutosha zilionekana hivyo, zaidi ya zile wanawake wanazovaa juu ya vichwa vyao namna hiyo, wameketi huko nje, na . . .

225 Imekuwaje kwa ulimwengu huu? Kuna nini? Loo, ewe kijana mwanamume, kijana mwanamke, jinyakue utoke kwenye hatua hiyo ya wendawazimu. Roho Mtakatifu aliwaongoza hapa, usiku wa leo. Inueni mikono yenu, na mumkubali Yeye kama Mwokozi wenu binafsi, usiku wa leo. Ataziondolea mbali dhambi zenu zote, na kuwapa furaha ambayo hamjui lolote kuihusu bado, mpaka mmemkubali Yeye. Si lazima uwe kijana, wazee wanaweza kufanya vivyo hivyo.

226 Katika maombi ya kumalizia, ni wangapi wangetaka kukumbukwa katika maombi, kwa kuinua mkono wako, na

kusema, “Nikumbuke, Ndugu”? Mungu akubariki. Mungu akubariki, kila mahali, hilo ni jema, kila mahali. Hilo ni jema.

²²⁷ Una haja moyoni mwako? Sema, “Mungu, ninakutarajia Wewe kunijibu katika uamsho huu. Nina watoto waliopotea. Nina baba aliyepotea, mama, ndugu, au dada, ama mpendwa, jirani, wakumbuke, Bwana.” Inua tu mkono wako. Yeye ata—Yeye—Yeye atasikia, Yeye atajua. Moyoni mwako tu, sema tu hilo. “Mwokoe huyu mpendwa.”

²²⁸ Sasa, kama umemwinulia mkono wako, basi nenda kamwite huyo mpendwa na uwaingize ndani. Waingizeni, hiyo ndiyo njia. Waleteni hapa, ili muweze kuwaleta kwenye Chemchemi, kama—kama vile Filipo alivyoenda na kumleta Nathanaeli kwa Bwana Yesu. Akamwambia mahali alipokuwa, chini ya mti, wakati alipompata.

²²⁹ Baba yetu wa Mbinguni, tuna furaha, usiku wa leo, kwa ajili ya majaliwa ya kusimama katika kanisa hili na kuwaombea watu. Tunashukuru kwa ajili ya Neno Lako, Neno Lako ni Uzima, Bwana. Nami naomba ya kwamba utatutumia uamsho tunaoombea.

²³⁰ Na sasa, Bwana, ninakuomba jambo fulani, binafsi, mimi mwenyewe: Tafadhali, Baba Mpendwa wa Mbinguni, weka ndani ya mioyo ya watu tarajio, jalia wasisahau hilo kamwe, kote usiku, kama tutaendelea katika mkutano, jalia wakumbuke usiku wa leo, wanautarajia.

²³¹ Tunakuja kila usiku. Sema, “Vema, haukutukia jana usiku, bali nitakuwa nikiutarajia kesho usiku, ita—itakuwa kesho usiku, itakuwa ni mimi. Mimi ndiye nitakayempokea Roho Mtakatifu. Mimi nitakuwa ndiye, wa kwanza madhabahuni kutubu dhambi zangu. Nitakuwa wa kwanza ambaye Mungu anatakasa na kuuondoa ulimwengu wote kutoka kwangu. Bwana, ninayaonea aibu maisha yangu, ninaona aibu jinsi nimekuwa nikifanya. Ni—ninataka uniondolee, unipe *kitu fulani* kikuu sana Bwana, hata sitataka kurudi kwenye kugaagaa huko kwa nguruwe tena, kama vile Biblia inavyosema dhahiri, ‘Kama nguruwe anavyorudi kwenye kugaagaa kwake, na mbwa kwenye matapiko yake.’” Nasi tunaweza kuona Bwana, ya kwamba wengi wa Wapentekoste wanatenda vivyo hivyo, kuondoka ulimwenguni, na kurudi moja kwa moja ndani yake tena.

²³² Mungu, tafadhali, jalia wasifikirie, Bwana, ninajaribu kuwakemea, lakini ni kujaribu tu kuweka Maandiko mbele yao, itawabidi kutembea juu Yake, Bwana, na kuyasukumia kando wapate kwenda mbali zaidi. Ninaomba ya kwamba kila mtu, na mimi mwenyewe, na sisi sote, tutayachunguza maisha yetu, na kuyalinganisha na matakwa ya Mungu. Tujalie, Baba.

²³³ Tusamehe dhambi zetu, utusamehe maovu yetu na makosa yetu. Jalia Damu ya Bwana Yesu ilitakase kanisa hili dogo, usiku wa leo. Ee Mungu, jalia kila mtu humu ndani apate m—mguso

wa Roho Mtakatifu, moja kwa moja, Baba. Tujalie. Jalia aje, tunaomba utujalie, Bwana, na kuanzisha uamsho papa hapa katika jiji hili. Tujalie, Bwana.

²³⁴ Lifanye kanisa hili kielelezo, ka—kanisa kielelezo. Na jalia watu waje kutoka sehemu mbalimbali na waangalie humu ndani na kuona jinsi mwenendo wao ulivyo, na jinsi wanavyojitenga na mambo ya ulimwengu, kurudi kwenye njia halisi, ya kweli, ya hakika ya Kipentekoste, ujuzi halisi, wa kweli wa Kipentekoste, wakitembea pamoja na Wewe, bila lawama. Tujalie, Bwana.

²³⁵ Ndipo makanisa mengine yataona, yatasema, “Vema, kama ndugu anaweza kufanya kanisa lake namna hiyo, na watu hao wote wanaweza kuwa pamoja, na mioyo yao inaweza kuwa kitu kimoja, na—na wamemnyoshea kila mtu mkono, basi angalia kuna tofauti kiasi gani ndani yao!” Bwana, ndipo wataona njaa na kiu.

²³⁶ Wewe ulisema, “Ninyi ni chumvi ya dunia, lakini chumvi ikipoteza ladha yake, haifai kitu tena, ila kutupwa nje, na kukanyagwa chini ya miguu ya watu.” Mungu, si kwamba watu wangenisikia, ikiwezekana funga masikio yao, na—nataka kusema hivi, Baba: Ninaangalia jinsi kanisa la Kipentekoste linavyoendelea, Ee Mungu, likikiri utakatifu, nasi tumekuwa nini? Chumvi iliyopoteza ladha yake.

²³⁷ Mungu, rudisha ladha nzuri kwenye chumvi upesi, ipate kuugusa ulimwengu huu unaoza, ili iweze... Ni ladha nzuri kama ikigusa, na ina Uzima ndani yake, itaokoa. Mungu, tufanye ladha ya ulimwengu, tujalie, Bwana. Weka ladha ndani yetu kulitia nguvu kanisa, ili watu waweze kuingia katika mlango huu na kuona nguvu za kufufuka kwa Bwana Yesu zikitenda kazi miongoni mwa watu, akijionyesha Mwenyewe yu hai milele.

²³⁸ Jalia tusiangalie kushangiliwa na watu, ama maoni ya watu, ama elfu arobaini katika mkutano wa kufanya uamsho, Ee Mungu, huo si uamsho. Ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu ataishika mioyo michache, na kulitikisa kanisa, na kusababisha uamsho halisi wa Kipentekoste. Tujalie, Bwana.

²³⁹ Uliahidi kusikia maombi, nami ninaamini utayasikia, ninapoikabidhi ibada Kwako, na hawa watu Kwako, upate kuyajibu maombi yetu, na kutimiza shauku zetu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁴⁰ Hebu tuimbe wimbo huu mzuri wa kanisa, ninaupenda tu, ni mmoja wa nyimbo ninazozipenda sana. Tupe sauti, “Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza, akanunua wokovu wangu pale Kalvari.” Mnaujua? [Ndugu Branham anasafisha koo lake—Mh.] Samahani.

Nampenda . . .

Sasa hebu na tuabudu, tumekuwa na ujumbe unaokatakata, hebu tuabudu.

...mpenda
 Kwani alinipenda kwanza
 Na kununua wokovu wangu
 Mtini Kalvari.

²⁴¹ Sasa hebu, tunapouimba tena, peaneni mikono, mtu aliye mbele yako, nyuma yako, bado hatujaruhusiwa kuondoka, sasa peaneni tu mikono, tunapoimba. Peana mikono na Wamethodisti, na Wabaptisti, na Umoja, na Uwili, na Church of God, na Assemblies of God, na Foursquare; sisi sote ni Foursquare. Hebu—hebu na tuweke mipaka yetu ng'ambo ya kizuizi chochote cha kimadhehebu, na tuwe ndugu.

²⁴² Ninawaona walioketi humu ndani, usiku wa leo, ninawatambua wengine, rafiki Mkatoliki, ninamwona mwingine, ndugu wa Dunkard, ndugu wa Kiamishi, na namna hiyo aliyeketi hapa, usiku wa leo. Sisi sote ni mmoja, kwa Roho mmoja sote tumenyweshwa kutoka kwenye Chemchemi moja.

Nampenda...
 Kwani alinipenda kwanza
 Na kununua wokovu wangu
 Mtini Kalvari.

²⁴³ Sasa, wakati mwingine maneno hayo huchoma sana na kwa nguvu, lakini kumbukeni, mnaona, tumetahiriwa, huko ni kukata mafundo, mnaona, tunatahiriwa kwa Neno la Mungu. Nalo linakata, bali ni zuri kwako, linakuchonga. Kata mti tena nao utazaa vizuri zaidi, usiache sehemu nyingi sana legevu zitoke kwake.

²⁴⁴ Hiyo ndiyo shida siku hizi, tuna sehemu nyingi mno zilizolegea, zinazoelekea *huku* na *huku*, jamii nyingi kupita kiasi, na nyingi sana za *hizi*, na nyingi sana za *zile*, hebu turudi kwenye jambo moja, Kalvari, ambapo tunaweza kuimba kwa moyo wetu. Nawe kadiri unavyojifanya mnyenyekevu zaidi...

²⁴⁵ Ni—ninaendelea tu, ninajaribu kukwepa hoja fulani hapa, nitaisema. Mkutano wangu wa mwisho huko Tucson, Arizona, siku tatu ama nne usiku zilizopita, niliwaona wazungu wakiingia mle, wagumu, Wapentekoste, wagumu walivyoweza kuwa; Niliwaona maskini Wameksiko wakiingia mle, walikuwako asubuhi ile nilipozungumza kwenye ibada ya asubuhi, waliketi mumo humo katika kanisa hilo siku nzima, kuanzia saa tatu asubuhi hiyo mpaka, vema, ilikuwa ni saa mbili, yapata saa moja, nadhani, ama saa mbili, walipoingia, nao wakaketi na kukaa moja kwa moja humo kanisani mpaka jioni hiyo.

²⁴⁶ Basi wakati ulipowadia, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka ndani ya hilo jengo, ni nani aliyeponywa? Wahispania, Wameksiko. Roho Mtakatifu akipitia moja kwa moja kwenye kusanyiko na kuwainua wagonjwa na wanaoteseka, na kila kitu

namna hiyo, akiwaleta huku, Wahispania, wanyenyekevu. Njoo ukiutarajia, hakuna kitu cha ulimwengu, ukimtaazama tu Kristo.

²⁴⁷ Nilikuwa Ujerumani, hivi majuzi. Ndugu Arganbright, mmoja wa ndugu zenu wa California hapa, Wafanyabiashara Wakristo, ninaamini yeye ni katibu, ama kitu fulani, ama mweka hazina, *kitu fulani* katika Wafanyabiashara Wakristo, mmoja wa wasimamizi wao, ndugu mzuri sana, hayuko hapa usiku wa leo, la sivyoy angekuwa jukwaani. Miner Arganbright ni mwaminifu kabisa, yeye ni mtu mzuri, unaweza kuweka tumaini lako kwa Miner Arganbright kama Mkristo. Nimekuwa pamoja naye katika mikutano ya kila namna.

²⁴⁸ Alikuwa ameketi pale usiku huku wachawi kumi na watano kila upande, wakijaribu kulipulia mbali kitu hicho, na kuona pale dhoruba ikiinyanyua, yapata watu thelathini au arobaini elfu, hema hilo likitikisika, hao wachawi wakikatakata unyoya huo, na kuuelekeza kwangu, pamoja na hayo makasi, huku wakipitia pale na kuimba, na kusema wangeita dhoruba, walifanya hivyo. Kamwe usiwadharau. Kwa hiyo wakaita dhoruba, kasema, “Tutailipulia mbali.” Huku mahali hapo pakubwa pakipanda juu chini namna *hiyo*.

Nikasema, “Ndugu Arganbright, omba.”

Nikasema, “Ndugu Lowster, usitafsiri haya.”

²⁴⁹ Nikasema, “Bwana Mungu, nilishuka kwenye ndege ile hivi majuzi, katika Jina la Bwana Yesu. Uliniambia ungenitetea wakati wa shida, kamwe huanipungukia bado, kwa hiyo, Bwana, umati huu wote umesisimkwa kabisa, kuna mamia na maelfu ya wakomunisti walioketi hapa,” na maskini msichana huyo kipofu alikuwa ndio kwanza aponywe, nikasema, “Ni Wewe, Mungu, Wewe unaweza kuliondoa hilo wingu, kwa hiyo ninalikemea hilo wingu.”

²⁵⁰ Mungu akiwa ni Hakimu wangu, moja kwa moja katikati ya hilo hema, likaanza kuvunjika, kuondoka *hivi*, na chini ya dakika moja jua lilikuwa linawaka, ngurumo zikinguruma namna hiyo, nimesimama pale, naam.

²⁵¹ Nami nikawaona Waswisi. Waswisi kamwe hawakupata mateso, wao ni kama Wamarekani, wazuri, wamelishwa, jamani, wamejaa kiburi tu, kama utaele-..., uh, samahani tamshi hilo. “Sisi ni *Akina nanii*. Sisi ni Wazwingli. Sisi ni—sisi ni Walutheri, haitubidi kusikiliza upuuzi huo.” Nao maskini hao Wajerumani wamefinyiliwa kabisa. Tulihasabu mabasi mia moja na themanini yaliyojaa, hayo mabasi makubwa yenye kioo juu yaliyojaa watu, yakaingia mahali ambapo kuna yapata watu elfu hamsini wamekusanyika pamoja kule kwenye uwanja mkubwa wa michezo.

²⁵² Na wakati... Ilikuwa? Wakati Roho Mtakatifu alipoanza kushuka, kila mtu huko nje walikuwa ni hao Wajerumani aliowaita. Wakaachwa wameketi pale pale walipokuwa

wameketi, wangali katika maradhi yao, wangali katika dhambi yao, wameketi papo hapo, na kuwaponya hao Wajerumani waliokuja na matarajio, huku wameinua mikono.

²⁵³ Walikuwa wameteswa sana kufikia mahali fulani, hao Wakristo huko juu chini ya Hitler na kadhalika, walikuwa wamepigwa kufikia mahali hata iliwabidi kumtazamia Mungu wapate rehema. Loo, Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo.

²⁵⁴ Enyi marafiki, angalieni, msiache iwe ni ninyi. Njoni na matarajio, mwe tayari. Weka kando kila mzigo mdogo unaokuzinga kwa urahisi, na uje kwa unyenyekevu moyoni, ukimtarajia Mungu kutimiza Neno Lake, Yeye atalitimiza.

Nampenda . . .

Hebu tufunge tu macho yetu sasa, na kuinua mikono yetu.

. . . nampenda

Kwani alinipenda kwanza

Na kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

Na . . . (Asante, Bwana.) . . . Nampenda

Kwani . . .

Funga tu macho yako na uwazie kile Yeye alichokufanyia. Kwa imani weka mikono yako juu ya vishungi Vyake vyenye Damu, uhisu maumivu Yake, masumbuko Yake makali.

Kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

Na tusimame sasa, kwa miguu yetu.

Nampenda, na . . .

Mwabuduni sasa, inueni tu mikono yenu, na tumwabudu.

Kwani alinipenda kwanza

Na kununua wokovu wangu

Juu ya ninii ya Kalvari . . .

²⁵⁵ Hebu tuuvumishe Kwake. Angalieni pale Kalvari: Upepo unavuma, mgongo Wake umeshikamana na msalaba, Damu na mate usoni Mwake. Ninaenda kwa imani, Bwana, ninaangalia msumari huo miguuni Mwako, na mikononi Mwako, ninaweka mikono yangu juu ya jeraha hilo ubavuni Mwako, Ni—ninahisi machozi ya misumari. Ulikufa nipate kuishi, Bwana. Jalia nijiachilie, Bwana. Jalia nipoteze kiburi changu chote, na upumbavu wote maishani mwangu, jalia niuhisi moyoni mwangu usiku wa leo, Bwana, hebu kanisa hili liuhisi moyoni mwao. “Alinunua wokovu wangu pale Kalvari.”

²⁵⁶ Wewe ni Mwana-kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu, nami ndimi niliye mwenye dhambi, ondolea mbali dhambi zangu. “Ee Mwana-kondoo wa Mungu, naja!” Ninakuja nikikiri makosa yangu, ninakuja nikikiri maovu yangu, nami ninakiri ya kwamba sistahili kuishi, lakini, Bwana, jalia niishi

kwa ajili Yake aliyekufa kwa ajili yangu. Jalia niachane na mambo yote ya ulimwengu ili niweze kupatikana, katika Yeye, mtumishi wa kweli.

²⁵⁷ Libariki kanisa hili, Baba, tunapouvumisha wimbo huu Kwako katika mioyo yenye shukrani, tukiimba kutoka mioyoni mwetu, ulisema tukiimba mioyoni mwetu juu ya shangwe, kwa sababu mafuta ya furaha ya Mungu yanamiminiwa nafsini mwetu.

Nampenda . . .

Sasa, abudu tu moyoni mwako.

. . . Nampenda

Kwani . . . (. . . ? . . .) 

61-0207 Tarajio
First Assembly Of God Of Long Beach
Long Beach, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org